# JAMHURI YA KENYA

**WIZARA YA MADZI, USAFI WA MAZINGIRA NA UNYUNYIRIZAJI MAJI**

**Mradi wa Pwani wa Uhifadhi wa Madzi na Mabadiliko ga Hali ya Anga**
**(CRWSCRP)**

**Mkopo Namba: IDA 5543-KE**

**Mradi Namba: P145559**

# MPANGIRIRO NAMBA TAHU (RAP 3) WA

## MRADI WA BARABARA ZA MWACHE

**RIPOTI YA MWISHO**

**JULAI 2023**

# MUKHUTASARI WA MAMBO GA UMUHIMU

Serekali ya Kenya (GoK) yaphokera mkopo wa chipesa kulaa kwa Bengi ya Dunia kuchirira mfumo wa Muungano wa Chimaenderero wa Chimataifa (IDA), mkopo uo ni wa kutengeza shuhuli za Miradi tsini ya Mradi Ubomu wa Uhifadhi wa Madzi na Kudzikwamula kulaana na athari ga Mabadiliko ga Tabia Ntsi khwenye eneo rosi ra Pwani (K2). Umwenga kati ya yo Miradi ambayo yatambuliwa kahi za ufadhili uu ni Mtsara Ubomu wa Mahumizi manji sana ga madzi nao ni Mtsara ubomu wa Mwache ambao u tsini ya Miradi Kipaombele khwenye Ruwaza ya 2030 ya Kenya. Mtsara uu ubomu wa Mwache waangazirwa kukhala ni wa umuhimu Zaidi ni Wizara ya Madzi, Uhifadhi wa Mazingira na Unyunyirizadzi Madzi Mindani (MoWSI), Serekali Za Kaunti ya Kwale na ya Mombasa. Mtsara uu Ubomu wa Mwache phamwenga na shuhuli zosini ambazo zindatuwiriza zindatekelezwa ni Wizara Ya Madzi, Uhifadhi wa Mazingira na Unyunyirizadzi wa Madzi Mindani, (MoWSI), Idara ya Chitaifa ya Madzi kuchirira mwavuri wa Mradi Ubomu wa Uhifadhi wa Madzi na Kudzikwamula kulaana na athari ya Mabadiliko ga Tabia Ntsi khwenye eneo rosini ra Pwani (K2).

Mradi Ubomu wa Uhifadhi wa Madzi na Kudzikwamula kulaana na athari za Mabadiliko ga Tabia Ntsi khwenye eneo rosini ra Pwani (K2) waidhinishwa ni Halmashauri ya Bengi ya Dunia mwezi wa kumi na Mbiri tarehe 16, mwaka wa 2014. Lengo bomu ra kutekelezwa kwa uu mradi ni uhifadhi wa madzi na kuhakikisha khwamba ganapatikana chila wakati, kisha hatua khwa hatua kujenga uwezo wa kudzidhibiti na kujikwamula kulaana na madhara ga mabadiliko ga hali ya anga au tabia ntsi. Koonjeza upatikanadzi wa madzi kwa unji chila wakati phamwenga na mazingira safi khwenye eneo rosini ra Pwani, kuchirira:

- Koonjeza upatikanadzi na usambazaji wa madzi kwa unji khwenye eneo rosini ra Pwani khwenda mpaka ndani ya Mombasa; na
- Khwaanzisha na khwendereza Mradi wa Unyunyirizadzi wa Madzi Mindani ili ikale dza chielelezo cha kuighwa.

Malengo ga khwaanzisha mradi uu wa ujenzi wa Mtsara Ubomu wa Mwache ni kuboresha hali ya chiutsumi na Maisha ga atu osini ario khwenye Kaunti za Kwale na Mombasa kuchirira kuphunguza chiwango cha umasikini na khwaanzisha maenderero enderevu. Mtsara uu Ubomu wa Mwache wa kuhifadhi madzi manji sana undaanzishwa khwa ajili ya mahumizi na kusambazwa khwa raia osini na viwandani khosini, phamwenga na usambazadzi wa madzi kwa ajili ya unyunyirizadzi wa madzi mindani. Usambazaji uu wa madzi kwa raia, viwanda na unyunyirizadzi madzi mindani undatsangira phabomu ukuzi na maenderero chijamii na chiutsumi kahi za eneo zima ra Pwani na pato ra chitaifa kwa ujumula. Malengo manjine ambago ganafungamana na utekelezaji uu ni uhifadhi wa mufumo wa chimazingira na kuvugula sehemu za minda kwa ajili ya unyunyirizadzi madzi mashambani ili koonjeza uvyalishaji wa chakurya.

**Malengo Mabomu ga Mpangiriro wa Hahu (RAP 3) wa Kutsamisa na kutsakulira atu makalo maphya kwa ajili ya atu ambao aathirika na utekelezwaji wa muradi ni:**

i. Kwepuka au kuphunguza madhara mabomu ga utsamishadzi na kutsakula makalo mbadala chihalisi na chiutsumi kulaana na utsamishadzi. Pharatu ambapho kayindaidimikika khwepuka kutsamisa atu be mipangiriro yinahenza yiikwhe na yitekelezwe khwa utaratibu ufaao ili kuhakikisha mwenderezo wa miradi ya chimaenderero khuno ikale raslimali zinalaviwa ifaavyo ili uwekezaji wa aratu arioathirika na kutekelezwa kwa muradi afaidike.

ii. Aratu ambao andauswa kulaa khwenye makalo gao yinahenzekana ahusishwe chikamili chisha apewe mwanya wa kushiriki kahi za kupanga mipangiriyo ya kutsamiswa kulingana na kanuni ambazo zaorodheshwa kwenye jedwali ra OP 4.12

iii. Aratu ambao andauswa khwenye makalo gakhwao yinahenzekana asaidiwe khwenye juhudi za khwao za kuboresha viwango vyao vya Maisha na chiutsumi ama audzirwe viwango ambavyo akhala anaishi navyo kabila ya kutsamiswa au kabila ya khwanzishwa kwa utekelezwaji wa muradi, kati ya zizo hali mara mbiri ni mtsagule yiyatu hali ambayo yindakala bora ziadi kahi za ao atsamiswa.

iv. Phunguzani athari bomu ya chijamii na chiutsumi ya aratu atsamiswao ya kumiliki minda khwa kuchirira zo njira zituwirizazo:

a. Kuripha chikamili raslimali yosini ambayo yindakala yihangamizwa khwa kutsamisa atu;

b. Kuhakikisha kukhala shuhuli zosi za kutshamira makalo maphya zinatekelezwa kwa njira ya lwazu na kushauriana na khukhala osini ambao andaathirika na utsamishadzi ahusishwa na ana habari za chikamili ya chila chitu chendereracho; na

c. Kuboresha au kuaudzira viwango vya Maisha na Chiutsumi vya aratu ambao aathirika na utekelezwaji wa muradi.

v. Kulavya usaidizi wa ziada na nafasi za (k.m., mikopo, mafundisho, au nafasi za kazi) na kuboresha au kudumisha na kuaudzira uwezo wa khwao wa kudzikimu chiutsumi, viwango vya uvyalishadzi wa chakurya khwa aratu ambao andaathirika na utekelezwaji wa muradi na kuhakikisha khwamba kaauya nyuma chiutsumi au chimaisha ila ikhale hali za khwao zinaboreka Zaidi.

vi. Kulavya usaidizi wakati wa mchiro khwa ajili ya aratu ambao aathirika na utekelezwaji wa muradi vyoihenzekanavyo.

vii. Makadirio gafaago ganahenza gafanywe kwha wakati ufaao ili kujumulisha uwezo wa kudzikimu chimapeni, uvyaalishadzi wa chakurya na viwango vya Maisha.

Kanuni Muhimu za Mpangiriro uu wa Uhamishadzi na kutsakulira Makalo mbadala (RAP) zinafungamana na irivyoorodheshwa kwenye OP. 4.12 na inajumuisha vipengele vituwiravyo: -

i. Kuaripha atu na kuapa atu makalo mbadala kwa ajili ya aratu arioathirika na utekelezwaji wa muradi kundatengezwa kulingana na sheria za Kenya na Sera za Bengi ya Dunia OP 4.12

ii. Pharatu ambapho sheria za Kenya kazindaapendelea aratu arioathirika na utekelezwaji wa muradi kuriko kanuni za Bengi ya Dunia, be phapho ndhipho kanuni za Bengi ya Dunia OP 4.12 ndizo ambazo zindatuwirizwa;

iii. Aratu ambao andaathirika chihalisi khwa makalo gao gapindi au chiutsumi andaphewa mwanya wa kutsagula kahi za kupewa utsamishadzi chikamili kutia ndani ardhi phamwenga na makalo au apewe pesa;

iv. Muradi undalavya mikakati ya kuhakikisha kukhala khuna mahumizi madzo ga pesa ambazo zindalaviwa kama fidia kwa aratu ambao andaathirika na utekelezwaji wa Muradi (Kuchirira Mafundisho ga Mahumizi ga Pesa) phamwenga na mipangiriro mahususi ga utuwiradzi ili kuhakikisha khwamba pesa za kufidiwa zindahumirwa tototo.

v. Chila nyumba ya aratu ambao andaathirika na utekelezwaji wa Muradi andasaidiwa kudumisha hali yakhwao ya chimaisha kuchirira kutekelezwa khwa mikakati ambayo indalenga kuhakikisha khwamba familia zinadumisha uwezo wa khwao wa chiutsumi ili kudziendereza.

vi. Muradi unalenga kuhakikisha khwamba chila Familia ambayo yindaathirika ni utekelezwaji wa Muradi andakhala alengwa abomu a Muradi; na khwamba mipangiriro yosini inaalenga kuafaidi ili kuaudzira hali ya khwao ya chiutsumi ikale dza viratu ambavyo akala kabila utekelezwaji wa Muradi ama bora Zaidi.

vii. Kundakhala na uwazi kahi za kutuwiriza na utathmini wa shuhuli zosini ambazo zindatekelezwa kahi za Muradi uu. Matokeo na manufaa ga Muradi uu pia gandaikwa lwazu..

viii. Yo Njira bomu ambayo yindahumirwa za mashauriano na jamii zindatia ndani kuiha jamii kahi za vikundi vidide vidide ili kuhenda mazungumzo, kundakala na mahojiano ga mwenga kwa mwenga na atu ario na habari za ndanindani zaidi kuhusiana na Muradi na Jamii khwa ujumula. Mashauriano gaga gandahendwa phatu ambapho phandatsagulwa chimberembere chisha phakhale phakubaliwa ni ashiriki na mapema.

**Vipengele Muhimu vya Muradi wa Mtsara ubomu wa Mwache na Mipangiriro ya Kutsamisa na kutsakhula Makalo mbadala kwa aratu atu ambao andaathiriwa ni Utekelezwaji wa Muradi (RAPs)**

Mpangiriro/Mkakati wa Khwanza (RAP 1)

Mpangiriro wa Khwanza (RAP 1) unatia ndani sehemu zituazo;

1. Sehemu ya Mtsara Ubomu ambayo inatia ndani;
   - Phatu pha kuhifadhi madzi (Phatu phenye timbo ya mawe gafaago jerijeri ambago gandahumirwa khwa ujenzi phapatikana kare. Mawe gago gandahumirwa kugandaganda sehemu ya china chibomu cha Mtsara ili itsivudze madzi).
   - Phatu pha Kambi bomu ya Muradi
2. Phatu pha shuhuli ambazo zindasaidia kufanikisha utekelezwaji wa Muradi wa Mtsara ambazo zinatia ndani sehemu ya kusafisha madzi na mabomba ga usambazaji khwa ajili ya mahumizi ga anadamu, chituo cha Polisi na Chiliniki au Chituo cha Afya.
3. Phatu pha mutsara udide upande wa tsini ambapho phanajumulisha phatu pha kumwaga mitsanga ambao undakala usala baada ya madzi kuphunguka sipidi
4. Barabara za kuchirira za aina tafauti tafauti A, F, H, C, G na J.

Mpangiriro/Mkakati wa Khwanza (RAP 1) igaviwa Zaidi katika sehemu mbiri RAP 1a na RAP 1b;

Sehemu ya khwanza RAP 1a inatia sehemu zosini za umuhimu ubomu wa Muradi uu ambayo inatia ndani Mtsara Ubomu, mtsara wa kuphunguza kasi ya madzi ya tsini na sehemu ya Timbo ya mawe ambazo zisehemu ya Renji ya Mwavumbo, Sehemu ya Mtsara Ubomu ina eneo andamizi ambaro rindasaidia ufanikishaji wa kutekelezwa kwa Muradi.

Sehemu ya Umuhimu Ubomu ya Phiri (P2) inatia ndani sehemu ambazo zinazunguluka Mtsara Ubomu ambazo zinajumulishwa khwenye sehemu bomu ya Hahu (P3), sehemu ya kufanikisha shughuli ya Mtsara Ubomu, sehemu ya Mtsara Ubomu ambayo yindagandwagandwa ambayo ni ya Ukuta wa Mtsara Ubomu na barabara zakwhakwhe zosi mpaka sehemu ya Mtsara Ubomu ya tsini ya kuphunguza kasi ya madzi na Barabara za kuchirira C, H, A3 na J.

Sehemu ya Phiri ya Mpangiriro (RAP 2) inatia ndani shuhuli zosini zihusianazo na utsamishadzi wa atu khwenye sehemu ya Mtsara Ubomu ya dzulu ya kuphunguza kasi ya madzi na barabara zosi zizungulukazo yiyo sehemu ya Mtsara Ubomu, na sehemu ya mtsara udide wa dzulu ra kuphunguza kasi ya madzi.

Sehemu ya Mpangiriro wa Hahu (RAP 3) inatia ndani Barabara A, D na E.

**Hali Halisi ya Utekelezwaji wa Shuhuli za Muradi (RAP) na Shuhuli Zosini ambazo Zinahusiana na Muradi.**

Ili kudziambatanisha na Mipangiriro ambayo yaikhwa mapema, iriyoidhinishwa na kuikhwa lwazu RAP, Wizara Ya Madzi, Uhifadhi wa Mazingira na Unyunyirizadzi wa Madzi Mashambani (MoWSI) kuchirira Tume ya Chitaifa ya Ardhi (NLC) yapata Hekta 946 (Ha) au Ekari 2,335 (Acres) kulaana na vipande vya ardhi 710 kulaa kwa Sehemu ya Khwanza (P1) na Sehemu ya Phiri (P2) ambazo ni sehemu ya RAP 1. Katika shuhuli zosi zizi za kupata ardhi khwa ajili ya utekelezwaji wa Muradi, Tume ya Ardhi Ya Chitaifa (NLC) yahenda kazi mwenga khwa mwenga na ahenzi a kazi a Wizara Ya Madzi, Uhifadhi wa Mazingira na Unyunyirizadzi wa Madzi Mashambani (MoWSI/PMU), Frontman Ltd (Ashauri a Utekelezaji wa Mradi RAP 1), Geomatics Surveyors (Masoroveya ga Ardhi ya Muradi), Akide Advocates (Mawakili ga Ufuatilizi wa Urithi wa Ardhi katika sehemu ya Muradi), na ahenzikazi a Idara ya Chitaifa ya Ardhi na Mipangiriro ya Makalo na Serekali ya Kaunti ya Kwale. Shuhuli na mipangiriro ambayo yatengezwa kufikira vivi yajumuishwa na yichiikwha lwazu kwa Mpangiriro ya Kutsamisa atu na kutsakula Makalo mbadala (RAP), ni khama ituwiriravyo :- Kubuniwa na khwaanzishwa khwa mfumo wa kuphokera na kusuluhisha malalamishi, Mpangiriro wa china wa Usoroveya, Ukaguzi wa Raslimali zosini khwenye ro eneo ra Muradi, Uchunguzi wa chiujumula, Kukabidhi stakabadhi za maripho za kufidia aratu ambao andauswa kulaa khwenye  makalo gao, Kufidia aratu ambao andaaathirika kulaana na utekelezwaji wa Muradi ili ardhi ikabidhiwe rasmi kwa Wizara Ya Madzi, Uhifadhi wa Mazingira na Unyunyirizadzi wa Madzi Mashambani (MoWSI). Baada ya kupatikana kwa ardhi chikamili kahi za yo mipangiriro ya P1 na P2 na kukabidhiwa chirasmi kwa Mwanakandarasi kwa ajili ya utekelezwaji wa Mruadi, vivi sambi matso gosi ganaerekezwa khwa kumiliki ardhi na matayarisho khwa ajili ya utekelezwaji wa sehemu zinjine ambazo zinahusiana na ujenzi wa Mtsara Ubomu.

Kwha wakati huu mkazo unaerekezwa khwenye khwaanzisha shuhuli za kuaudzira aratu arioathirka na utekelezwaji wa Muradi khwenye Sehemu ya Khwanza P1 na Sehemu ya Phiri P2 hali yao khwao ya chiutsumi na ili adzikimu chimaisha. Khwa ajili ya Sehemu ya Hahu P3 vipande vya ardhi 968 vindahenzekana khwa ajili ya kutengeza ukuta wa Mtsara Ubomu na phatu pha kumwaga mtsanga undiorichwa ni madzi baada ya madzi kuphunguka kasi ya khwakhwe kuko sehemu ya tshini ya Mutsara Ubomu.

**Mipangiriro ya Kumiliki Ardhi khwa ajili ya Barabara za Mtsara Ubomu wa Mwache**

Mradi wa Mtsara Ubomu wa Mwache unahusisha barabara chenda (9). Sehemu ya Hahu ya Utekelezwaji wa Muradi (RAP 3) inalingana na michoro ya Barabara ambayo yakhala yilaviwa pindi ni ye Mteja ambaye ni Wizara Ya Madzi, Uhifadhi wa Mazingira na Unyunyirizadzi wa Madzi Mashambani (MoWSI), kuchirira kwa yiye Injinia Mwiimirizi wa Mtsara Ubomu. Matayarisho ga Mpangiriro wa Hahu RAP 3 unatuwirizira Mpangiriro wa Kwanza RAP 1 na wa Phiri RAP 2 ili khweelepha muphenyererano wa chimipangilio. Baadhi ya barabara zizo zi ndani ya Mpangiriro wa Kwanza RAP 1 na zinjine zachorwa ili zijengwe khwenye ardhi ambayo yi khwenye Mpangiriro wa Phiri (RAP 2). Hata vivyo Mpangiriro wa Hahu RAP 3 udzidziimisa chihicheye ili kushuhulikira barabara zosi ambazo zindajenghwa au kuboreshwa tsini ya Muradi wa Mtsara Ubomu wa Mwache hata chikala zalangazirwa khwenye Mpangiriro wa Kwanza RAP 1 ama wa Phiri Rap 2.

**Jedwali ra Kwhanza (A): Muhtasari wa Barabara tshini ya Muradi**

| # | Barabara | Maelezo yakalako/ Mbiphya | Sehemu ya iriphoandikishwa au Upimadzi wa Ardhi | Walamu (Mita) (Pharatu ambapho inabidi) | Ure Kilometa (Km) | Mpangiriro /Mkakati (RAP) Uhusikao kahi za kumiliki Ardhi/Undiohumika ili kumiliki Ardhi (Pharatu ambapho inabidi) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | A | Ni ya pindi (Kufikira daraja ra SGR) na sehemu zinjine ambazo zapatikana tsini ya Mpangiriro wa Khwanza RAP 1 | Sehemu ya Waandishi ya Mazeras | Sehemu bomu ya barabara yiyi yindaboreshwa kwa kuhumira Mpangiriro urioko wa umiliki wa Ardhi wa Sehemu ya khwanza na ya Phiri RAP 1; Chitengo Muhimu cha Khwanza na cha Phiri P1 na P2. Ardhi ziada ***Hekta 0.29 indahitajika na indapatikana kulaa kwa chipande cha ardhi*** | 5.151 | Sehemu ya Khwanza RAP I na Sehemu ya Hahu RAP 3 |
| | | | | ***tsini ya Sehemu ya Hahu RAP 3.*** | | |
| 2. | B | Iriyoko | Sehemu ya Upimadzi ya Mnyenzeni | Sehemu bomu ya barabara yiyi yindaboreshwa kwa kuhumira Mpangiriro urioko wa umiliki wa Ardhi wa Sehemu ya khwanza na ya Phiri RAP 1 na | 5.359 | Kakuna Ardhi ya ziada yindiyohitatajika tshini ya sehemu zosi Tahu za Mipangilio ya Utsamishaji. |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | RAP 2; Khakuna yoyosini ya ardhi ya ziada ambayo yindahitajika | | |
| 3. | C | Yiyi ni sehemu mbiphya lakini yikhwenye ardhi yiriyo khwenye Mpangiriro wa Khwanza RAP 1 | Sehemu ya Waandikishaji ya Mazeras | **Mita 20;** Barabara yiyi yindajengwa khwenye ardhi ambayo tayari yamilikiwa khare katika Mpangiriro wa Kwanza RAP 1; Khakuna. Ardhi ya ziada indiyohitajika | 0.842 | Mpangiriro wa Khwanza RAP I |
| 4. | D | Mbiphya | Sehemu ya Upimadzi ya Mnyenzeni | **Mita 20;** Hekta 1.31 ya Ardhi indahitajika kulaa khwa vipande vitsano vya ardhi tsini ya Mpangiriro wa Hahu RAP 3. | 1.120 | Mpangiriro wa Hahu RAP 3 |
| 5. | E | Kuna Sehemu ya Pindi na Sehemu Mbiphya | Sehemu ya Waandikishaji wa Mwavumbo na Chigato Na Sehemu ya Upimadzi ya Mnyenzeni | **Mita 40 hadi 60;** Hekta 53 zindahitajika kulaa khwa vipande 233 vya ardhi tsini ya Mpangiriro wa Hahu RAP 3. Ardhi Yindahumika ili kualamusa sehemu ya Barabara na kuvugula uphya chiwanja chiphya kwa ajili ya ujenzi wa barabara | 15.556 | Mpangiriro wa Hahu RAP 3 |

| # | Barabara | Maelezo yakalako/ Mbiphya | Sehemu iriphoandikishwa au Upimadzi wa Ardhi | Walamu (Mita) (Pharatu ambapho inabidi) | Ure Kilometa (Km) | Mpangiriro /Mkakati (RAP) Uhusikao kahi za kumiliki Ardhi/Undiohumika ili kumiliki Ardhi (Pharatu ambapho inabidi) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 6. | F | Yakalako kulaa hangu pindi | Sehemu ya Waandikishaji ya Chigato | Barabara yindaboreshwa kulaa khwa barabara iriyoko vivi tsini ya Mpangiriro wa wakati uu wa Barabara. **Kakhuna Ardhi ya ziada ambayo yindahitajika *kwa ajili ya ujenzi wa sehemu yiyi.*** | 3.945 | Khakuna Ardhi ya ziada yinndiyohitajika tshini ya sehemu zosi tahu za Mipangilio ya Utsamishaji. |
| 7. | G | Mbiphya (Barabara yiyi ni ya muda mfuti) ardhi ya khwakhwe yindalaa kwa sehemu ambayo yapatikana kulaa khwa Mpangiriro wa Khwanza RAP 1 | Sehemu ya Waandikishaji ya Mwavumbo na Chigato | **Mita 20;** Barabara yiyi yindajengwa kulaana na ardhi iriyopatikana kulaa khwa Mpangiriro wa Khwanza RAP 1; Chitengo cha 1 na 2. Kakhuna ardhi ya ziada ambayo yindahitajika kwa ujenzi uu. | 1.929 | Mpangiriro wa Kwanza RAP 1 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 8. | H | Mbiphya lakini kulaa khwa sehemu iriyopatikana kulaa kwa Mpangiriro wa Khwanza RAP 1 | Sehemu ya Waandikishaji ya Mazeras | **Mita 20;** Barabara yiyi yindajengwa kulaana na ardhi iriyopatikana kulaa khwa Mpangiriro wa Khwanza RAP 1; Chitengo cha 1 na 2. Kakhuna ardhi ya ziada ambayo yindahitajika kwa ujenzi uu. | 0.745 | Mpangiriro wa Khwanza RAP 1 |
| 9a. | UCD1-Barabara za kuchirira za vidzidzini | Ni Mbiphya lakini yindajengwa khwenye ardhi ambayo yapatikana khwenye Mpangiriro wa Phiri RAP 2. | Sehemu ya Upimadzi ya Bofu | **Mita 20;** Barabara yiyi yindajengwa kulaana na ardhi iriyopatikana kulaa kwa Mpangiriro wa Kwanza RAP 2 . Khakuna ardhi ya ziada yindiyohitajika | 0.7 | Mpangiriro wa Khwanza RAP 2 |

| # | Barabara | Maelezo yakalako/ Mbiphya | Sehemu ya iriphoandikishwa au Upimadzi wa Ardhi | Walamu (Mita) (Pharatu ambapho inabidi) | Ure Kilometa (Km) | Mpangiriro /Mkakati (RAP) Uhusikao kahi za kumiliki Ardhi/Undiohumika ili kumiliki Ardhi (Pharatu ambapho inabidi) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | | | kwa ajili ya sehemu yiyi ya barabara . | | |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 9b. | UCD2-Barabara ya kuchirira ya upande wa kurya wa Mtsara Ubomu | Ni Mbiphya lakini indajengwa khwenye ardhi iriyopatika na khwenye Mpangiriro wa Phiri RAP 2 | Sehemu ya Upimadzi ya Bofu | **Mita 20;** Barabara yiyi yindajengwa kulaana na ardhi iriyopatikana kulaa khwa Mpangiriro wa Phiri RAP 2 . Khakuna ardhi ya ziada ambayo yindahitajika khwa ajili ya sehemu yiyi ya Barabara kulaa khwa Mpangiriro wa Hahu RAP 3 | 1.2 | Mpangiriro wa Kwanza RAP 2 |
| 9c. | UCD3-Barabara yeerekezayo khwenye Sehemu ya umwagaji wa taka kulaa khwa Mtsara Ubomu | Ni Mbiphya lakini yindajengwa khwenye ardhi iriyopatika na khwenye Mpangiriro wa Phiri RAP 2 | Sehemu ya Upimadzi ya Bofu | **Mita 20;** Barabara yiyi yindajengwa kulaana na ardhi iriyopatikana kulaa khwa Mpangiriro wa Phiri RAP 2 . Khakuna ardhi ya ziada yindiyohitajika khwa ajili ya sehemu yiyi ya Barabara kulaa khwa Mpangiriro wa Hahu RAP 3 | 1.6 | Mpangiriro wa Phiri RAP 2 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 9d. | UCD4-Barabara ya kuchirira ya khwenye Mtsara Ubomu | Ni Mbiphya lakini yindajengwa khwenye ardhi iriyopatikana khwenye Mpangiriro wa Phiri RAP 2 | Sehemu ya Upimadzi ya Bofu | **Mita 20;** Barabara yiyi yindajengwa kulaana na ardhi iriyopatikana kulaa khwa Mpangiriro wa Phiri RAP 2 . Khakuna ardhi ya ziada ambayo yindaohitajika kwha ajili ya sehemu yiyi ya Barabara kulaa kwha Mpangiriro wa Hahu RAP 3 | 1.0 | Mpangiriro Namba Mbiri RAP 2 |
| 9e. | UCD5-Barabara ya kuchirira dzulu ya Mtsara Ubomu | Ni Mbiphya lakini yindajengwa khwenye ardhi yiriyopatikana khwenye Mpangiriro wa Phiri RAP 2 | Sehemu ya Upimadzi ya Bofu | **Mita 20;** Barabara yiyi yindajengwa kulaana na ardhi iriyopatikana kulaa kwa Mpangiriro wa Phiri RAP 2 . Khakuna ardhi ya ziada yindiyohitajika khwa ajili ya sehemu yiyi ya Barabara kulaa khwa Mpangiriro wa Hahu RAP 3 | 0.2 | Mpangiriro wa Phiri RAP 2 |

| # | Barabara | Maelezo yakalako/ Mbiphya | Sehemu yiriphoandikishwa au Upimadzi wa Ardhi | Walamu (Mita) (Pharatu ambapho inabidi) | Ure Kilometa (Km) | Mpangiriro /Mkakati (RAP) Uhusikao kahi za kumiliki Ardhi/Undiohumika ili kumiliki Ardhi (Pharatu ambapho inabidi) |
|---|---|---|---|---|---|---|
| 9f. | UCD6-Barabara za kuunganisha sehemu za tsini ya Mtsara Ubomu | Ni Mbiphya lakini yindajengwa khwenye ardhi iriyopatikana khwenye Mpangiriro wa Phiri RAP 2 | Sehemu ya Upimadzi ya Bofu | **Mita 20;** Barabara yiyi yindajengwa kulaana na ardhi iriyopatikana kulaa khwa Mpangiriro wa Phiri RAP 2 . Khakuna ardhi ya ziada yindiyohitajika kwa ajili ya sehemu yiyi ya Barabara kulaa kwa Mpangiriro wa Hahu RAP 3 | 0.3 | Mpangiriro wa Phiri RAP 2 |
| 9g. | UCD7-Barabara za kufisha khwenye vyemba vya kuvugulira madzi | Ni Mbiphya lakini yindajengwa khwenye ardhi iriyopatikana na kwhenye Mpangirir | Sehemu ya Upimadzi ya Bofu | **Mita 20;** Barabara yiyi yindajengwa kulaana na ardhi yiriyopatikana na kulaa khwa Mpangiriro wa Phiri | 0.2 | Mpangiriro wa Phiri RAP 2 |

| | | | | | | |
|---|---|---|---|---|---|---|
| | | o wa Phiri RAP 2 | | RAP 2 . Khakuna ardhi ya ziada yindiyohitajika kwa ajili ya sehemu yiyi ya Barabara kulaa khwa Mpangiriro wa Hahu RAP 3 | | |

*(i) Barabara ya Khwanza (A- Barabara ya kuuunganisha mpaka sehemu ya Mtsara Ubomu)*

Yiyi barabara yinaanzira kulaa khwenye Barabara bomu ya Mombasa – Nairobi kulaa Mazeras pho phenye matanyiko ga khwenda Chinango, Inachirira Mazera Misheni mpaka kufikira Daraja ra Reli ya Chisambi (SGR) mkabala na sehemu ya Mtsara Ubomu wa Mwache. Yiyo sehemu ya barabara yiriyo phephi na Daraja ra Reli ya Chisambi mkabala na Mtsara Ubomu wa Mwache ambayo tayari yapatikana katika Mpangiriro wa sehemu ya khwanza yaani RAP 1. Yiyi barabara yina ure wa kama kilomita 5.2. Inaanzira phapho Mazeras baada tu ya kurichana na Barabara bomu ya Mombasa – Nairobi mpaka khwenye sehemu yihenderwayo kazi ya Mtsara Ubomu. Sehemu bomu ya yiyi barabara yindaboreshwa kuchirira Mpangiriro ambao tayari ukhwenye urekebishaji wa barabara katika ardhi ambayo tayari inamilikiwa kuchirira Mpango wa RAP 1, sehemu ya umuhimu ya khwanza na ya phiri P1 na P2. Hata vivyo ardhi ya ziada ikadiriwayo khukhala Hekta ***0.29 yindahitajika na yindapatikana kulaa kwa chipande chimwenga cha ardhi ambacho chitsini ya Mfumo wa Hahu wa chimikakati yaani RAP 3.***

Sehemu ya Khwanza ya Barabara (A1): Kulaa Mazeras Madukani mpaka Sukuli ya Sokondari ya Mazeras.

- Sehemu yiyi ya Barabara yina ure wa Kilomita 1.7
- Sehemu yiyi ya barabara yindatiywa kokoto dza irivyo kwa sambi na khakhuna ardhi ya ziada yindiyohitajika.;
- Majengo ga Biashara ambago ga mkabala na barabara ndizo ambazo zatengezerwa makadirio ga kufidiwa, majengo gaga ni garatu ambago ga khwenye sehemu ya phiri ya barabara yaani kulaa Sukuli ya Sokondari ya Mazeras mpaka khwenye Daraja ra Reli ya Chisambi ya SGR.
- Sehemu yiyi ya phiri yina ure wa kilomita 1.4
- Sehemu ya Hahu (A3) yindatiywa Lami ambayo yinaanzira khwenye daraja ra Reli ya Chisambi SGR mpaka sehemu ambayo yinahenderwa kazi ya Mtsara Ubomu wa Mwache.
- Yiyi sehemu ya barabara yina ure wa Kilomita 2.1 na yindahumika khwa ajili ya kufikira sehemu zosi za Mtsara Ubomu zihenderwazo kazi kwa urahisi
- Sehemu yiyi ya ardhi tayari yapatipatikana na aratu atu orokala anaishi khwenye yiyi ariphiwa kare na achitsama.

*(ii) Barabara ya Phiri (B- ni Barabara yiriyo khwenye sehemu ya Mkono Kurya wa Mtsara Ubomu)*

- Yiyi barabara tayari yiphapho na yindahitaji kuboreshwa kuchirira Mpangiriro urioko tayari wa udumishaji wa barabara, khakuna ardhi ya ziada ambayo yindahitajika tshini ya Mfumo wa Chimikakati wa Hahu yaani RAP 3.
- Yiyi barabara ina ure ambao unakadiriwa kukala kilomita 5.4. Yiyi barabara inalaa khwenye barabara ya Mazeras – Kinango (D560) na yinatengeneza mkunzo wa duara kuzunguluka sukuli ya Msingi ya Miyani halafu inauya tena khwenye barabara ya Mazeras – Kinango
- Sehemu bomu ya yiyi barabara i khwenye eneo ra ardhi ririropimwa ra *Mnyenzeni*

*(iii) Barabara ya Hahu (C – Barabara ya kufisha khwenye eneo ra Chituo cha kupigira madzi)*

- Yiyi ni barabara yifishayo khwenye chituo cha kupigira madzi
- Barabara yiyi yinakadiriwa kukhala na ure wa Kilomita 0.9 ndani ya eneo ra Mtsara Ubomu nayo yindaboreshwa kwa kutiywa kokoto.
- Yiyi barabara yindajengwa kwenye eneo ra ardhi ambaro tayari rapatikana tsini ya Mpangiriro wa Chimikakati Namba Mwenga yaani RAP 1, Chitengo chibomu cha khwanza P1. Kaphandakala na uhitaji wa kupata ardhi yinjine kuchirira Mpangiriro wa Chimikakati Namba Tahu yaani RAP 3 khwa ajili ya yiyi barabara. Yiyi barabara yindajengwa khwenye ardhi ambayo yapatikana kare tshini ya Mpangiriro wa Chimikakati Namba Mwenga RAP 1.

*(iv) Barabara ya Nne (D – Barabara ya kufisha khwenye sehemu ya dzulu Zaidi ya Mtsara Ubomu mkabala na Barabara ya Chinango)*

- Yiyi barabara khwa vivi kayipho na indakala khwenye sehemu mbiphya kabisa ambayo indahitaji kwaanzishwa luphya kulaa kutema musuhu. Sehemu fulani ya ardhi ya kujenga yiyi barabara tayari yakala yipatikana. Barabara yiyi yindaunganisha barabara ya Phiri na Mutsara Ubomu.
- Yiyi barabara yinakadiriwa kukhala na ure wa Kilomita 1.1 na walamu wa mita 20 na yindahitajika kutiywa Lami
- ***Chipande cha ardhi chipatacho Hekta 1.31 chindahitajika kulaa khwenye vipande vitsano vya ardhi kwa ajili ya ujenzi uu tshini ya Mpangiriro wa Chimikakati Namba Tahu yaani RAP 3.***

*(v) Barabara Ya Tsano (E- Utandazaji na urekebishaji wa Barabara D560)*

- Barabara yiyi ndiyo yindiyokhala barabara bomu ya kuunganisha Mazeras na Chinango. Yiyi barabara yinakadiriwa kukhala na ure wa kilomita 15.4 na kazi bomu ya yiyi sehemu yindakala ya kutandaza na kunyoroshwa kulingana na viratu ambavyo yakusudiwa kulaa hangu pindi D560.
- Yiyi barabara yina walamu upatao mita 40 – Isiphokala khwenye sehemu ya daraja ambayo yina walamu wa mita 60.

  • Barabara yiyi yinachirira sehemu nne za waandikishaji/Usajili wa ardhi ambazo ni Mazeras (Kilomita 1.5), Renji ya Mwavumbo (Kilomita 8.0), Chigato (Kilomita 4.0) na Mnyenzeni (Kilomita 2.0). Vipande vya ardhi katika sehemu ya Chigato tayari vyasajiliwa lakini mashamba ga kwenye sehemu ya Mnyenzeni saa yiyi ndo ga khwenye shuhuli ya upimadzi. Kwa sababu yiyo mashamba gapewa namba za kugwiririra kadiri shuhuli ya upimadzi unaenderera. Viratu vipande vya ardhi ambavyo vindahitajika khwa ajili ya Muradi tayari vyapewa namba za kugwiririra. Pia sehemu ya Renji ya Mwavumbo pia nayo ikhwenye shuhuli ya upimadzi wa ardhi, hata vivyo vipande vya ardhi ambavyo vindahitajika vyapewa namba za kugwiririra ili kusaidia kuendereza shuhuli za Mradi huu.

- Yiyi barabara yindatiywa lami hata ijapokuwa kuna sehemu ambazo ni njeni ambapho kakudzangwe kukhala na barabara pho pindi ambazo zikhwenye eneo ra Renji ya Mwavumbo
- Yiyi barabara yindahitaji sehemu za kandakanda yaani ardhi ya ziada kandakanda ya barabara ambayo indahitaji kugulwa. Yiyi ardhi ya ziada ndo yindahumika kualamusa barabara katika sehemu ambazo ni nyembamba na kuvugula sehemu ya ardhi ambayo kaidzangwe kujengwa kwa ajili ya kupanua barabara. Vipande vya ardhi 233 vindahitajika virivyo na ujumla wa Hekta ***53 tshini ya Mpangiriro wa Chimikakati wa Hahu yaani RAP 3.***

*(vi) Barabara ya Sita ( F – Yiyi ni Barabara ya Chidzidzi cha Chigato)*

- Yiyi barabara tayari yiphapho na yikhwenye eneo ra usajili wa ardhi ra Chigato.
- Yiyi barabara yindakarabatiwa ili ikhale katika Chiwango ambacho chakusudiwa kulaa hangu pindi na khakundakala na uhitaji wa kutsakula ardhi yinjine ya ziada tshini ya Mpangiriro wa Mikakati wa hahu RAP 3.
- Barabara yiyi yina ure wa Kilomita 4
- Kusudi bomu ra barabara yiyi ni kuhakikisha khwamba sehemu ya tshini ya Mtsara Ubomu yinafikika ambapho iyatu sehemu ya Mtsara Ubomu ya tshini ya kuphunguza kasi ya madzi yinafikika na pia yikale chiunganisha cha timbo ya mawe na kuchihenda chidzidzi cha Chigato chikhale na barabara za kuchirika.

*(vii)Barabara ya Sabaa (G – Yiyi ni barabara ya muda ufuti ili kuerekeza magari kulaa khwenye barabara bomu D560)*

- Yiyi barabara ni ya muda ufuti idzilavyayo kulaa khwenye barabara ya D560 ambayo yindahumika wakati wa ujenzi wa Mtsara Ubomu ambayo yinapatikana kwhenye sehemu ya Renji ya Mwavumbo na sehemu ya usajili wa ardhi ya Chigato phephi na daraja riririrokho ra Mwache.
- Yiyi barabara yina ure wa Kilomita tahu 3 na sehemu tide tu ya barabara ndiyo yindatiywa kokoto khwenye pande zosi;
- Yo Ardhi ambayo yiyi barabara yindajengwa tayari yapatikana tshini ya Mpangiriro wa Mikakati wa khwanza RAP 1; Sehemu ya umuhimu ya khwanza na ya phiri. Kwa vivyo khakuna haja ya ardhi ya ziada tshini ya Mpangiriro wa Mikakati namba Tahu yaani RAP 3.

*(viii) Barabara ya Nane (H – Barabara ya kufika kwhenye kambi ya tshini)*

- Yiyi barabara yinaunganisha sehemu ya tshini ambakho kuna kambi bomu na barabara ya kwhanza yina ure wa nusu Kilomita (0.5) na walamu wa Mita 20.
- Sehemu ya ardhi ya kujenga yiyi barabara tayari yapatikana tshini ya Mpangiriro wa Mikakati RAP 1; Sehemu ya umuhimu ya khwanza na ya phiri. Kwa vivyo khakuna haja ya ardhi ya ziada tshini ya Mpangiriro wa Mikakati namba Tahu yaani RAP 3.

*(ix) Barabara za kuunganisha sehemu ya dzulu ya Mtsara Ubomu ra kuphunguza kasi ya madzi.*

Kuna barabara nne ambazo zindaunganisha sehemu ya dzulu ya Mtsara Ubomu ra kuphunguza kasi ya madzi. Zizi barabara zosi zindakala na ure wa chijumla wa Kilomita 4.5 na walamu wa Mita 20.

**Mfikiro wa Mpangiriro wa Chimikakati Namba Tahu (RAP 3)**

Mpangiriro wa Chimikakati wa utsamishadzi na kutsakhula Makalo mbadala wa Hahu wa Mtsara Ubomu wa Mwache almaarufu (RAP 3) unajumuisha athari ambazo zindapatikana kulaana na kuphalwa khwa Hekta **54.61** za ardhi khwa ajili ya ujenzi na upanuzi wa Barabara A, D na E. Sehemu zinjine ambazo kazihusisha ardhi ya Makalo lakini zindaathiriwa katika Mpangiriro uu ni Majengo/Nyumba, Mihi, Mabira, na kuhangamiza pato ra chibiashara khwenye vipande vya ardhi ambavyo vindahitajika chilazima phamwenga na ziratu sehemu za ziada za barabara khwa ajili ya upanuzi na usawazishwaji wa barabara zirizoko kwa vivi.

Michoro ya barabara na sehemu ambatanishi ambazo zinahitaji kushuhulikirwa zakabidhiwa kare khwa Mshauri wa Mpangiriro wa Mikakati Namba Tahu (RAP 3). Injinia wa Wizara aimiriraye Mradi wa Mtsara Ubomu wa Mwache wamkabidhi zo stakabadhi zosini Mshauri wa Mradi na achimwonyesa sehemu ambazo zinahitaji kushuhulikirwa. Mshauri wa Mradi naye waphala michoro yosini chisha achiyiambatanisha na Ramani zirizoidhinishwa ambazo zapatikana kulaa khwa Idara ya Chiserikali ya Ardhi na Mipango. Baada ya kwaambatanisha michoro na ramani achitokeza Ramani ambayo inaonyesa chila Chipengele cha Mradi (Ramani za Cadastroli) dza ambavyo zinaoonyeswa khwenye Jedwali-andamizi ra phiri (Annex II) ambayo inaonyesa iyatu ardhi ambayo yindahitajika khwa ajili ya ujenzi wa barabara mbiphya.

**Mhutasari wa Athari na Hatari zihusianizo na utekelezwaji wa Mpangiriro wa Mikakati Namba Tahu (RAP 3) khwenye eneo ra Mradi.**

Eneo rosini ra Mradi wa Mwache rinakalwa ni jamii mwenga ambayo ni Aduruma ambao ni kabila mwenga kati ya makabila chenda ga amidzichenda ambao anaishi eneo ra Pwani. Aduruma atambuliwa kukhala abaki nyuma chimaenderero na khwamba anaishi khwenye mazingira makomu ambago ganahatarisha hali yao ya chimaisha. Ripoti yiyi yalaa khwenye ukaguzi uriofanywa kulaana na Stakabadhi ya Uhendaji Kazi wa Bengi ya Dunia 4.10. Katiba ya Kenya (CoK) 2010, pia nayo yayiika Kaunti ya Kwale kahi ya maeneo ambago gabaki nyuma Chimaenderero na khwamba anantsi akhwakhwe anaishi katika mazingira makomu.

Mpangiriro wa Mikakati Namba Tahu RAP 3 waorodhesha na koonyesha waziwazi kuchirira maandishi khwamba barabara zosi ambazo zina uhusiano na utekelezwaji wa ujenzi wa Mtsara Ubomu wa Mwache zindaathiri chihalisi na chiutsumi nyumba/famili 267 na atu 1,020. Atu ao anapatikana khwenye sehemu ambazo kazikhwenye barabara na anjine ambao anaishi kandakanda ya barabara zirizoko khwa vivi khare. Atu ambao anaishi khwenye midzi 19 indabidi auswe kamarekamare ende akatsakhule makalo manjine baada ya kuhangamiza midzi yao ambapho akala anaishi kulaa hangu pindi. Khwa vivyo achuuka andahangamizi ardhi, nyumba na majengo gao ga biashara.

Zo nyumba au Boma 267 zosi zaorodheshwa kukala kahi za hatari ya kuhangamiza makalo na uwezo wao wa kudzikimu chimaisha kwa sababu ya kufikisha vigezo virivyoorodheshwa khwenye Ripoti ya Bengi ya Dunia ambayo yinahusianishwa na Sera za Atu namba (OP4.10).

**Jedwali ra Phiri: Mgawanyiko wa Midzi au Nyumba na Atu andioathirika kulingana na Barabara**

| # | Barabara | Nyumba zindizoathirika | atu andioathirika | Vipande vya Ardhi |
|---|---|---|---|---|
| 1. | Ya Khwanza A | 4 | 20 | 1 |
| 2. | Ya Nne D | 5 | 30 | 5 |
| 3. | Ya Tsano E | 258 | 970 | 233 |
| | **Jumula** | **267** | **1,020** | **239** |

**Jedwali ra Hahu (C): Muhtasari ya Umbopande ya Athari**

| # | Aina ya Hasara | Idadi ya Nyumba/ Boma Zindizoathirika |
|---|---|---|
| 1. | Nyumba/Boma zindizohanganiza Zaidi ya Asilimia 20 ya Ardhi | 45 |
| 2. | Nyumba/Boma zindizohanganiza Tsini ya Asilimia 20 ya Ardhi | 155 |
| 3. | Nyumba/Boma zindizohangamiza Mihi | 74 |
| 4. | Nyumba/Boma zindizohangamiza Mimera hicheye | 0 |
| 5. | Nyumba/Boma zindizohangamiza biashara na nyumba za makalo | 19 |
| 6. | Nyumba/Boma zindizohangamiza sehemu zao za Mabira | 3 |

**Athari ya Ardhi indiyomilikiwa Khwa ajili ya Mradi**

Jumula ya Nyumba/Boma 239 zindahangamiza ardhi ya khwao kwa ujumula indakala Hekta **54.61**. Vipande vyosini vya ardhi vindivyophalwa kwah ajili ya Muradi zi tsini ya mahumizi huru ga chibinafsi.

**Jedwali ra Nne (D): Muhtasari wa Ardhi indivyoathirika**

| # | Barabara Zindizohitajika | Vipande vya Ardhi vindivyohitajika | Ubomu wa Ardhi kwa Hekta | Ure kwa Kilomita | Walamu khwa Mita (Jumula ya walaamu undiohitajika) |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Barabara ya Khwanza (A) | 1 | 0.29 | 5.15 | 20 |
| 2. | Barabara ya Nne (D) | 5 | 1.31 | 1.12 | 20 |
| 3. | Barabara ya Tsano (E) | 233 | 53.01 | 15.55 | 40-60 |
| | **Jumula** | **239** | **54.61** | **23.19** | |

**Athari za Ujenzi wa Barabara kanda na Ardhi**

Ujengaji wa barabara undakhala na athari ya chiutsumi na chihalisi kulaana na kutsamiswa kwa atu kulaa kwa ardhi ambayo adziishi kwa muda ure ili kuphisa nafasi ya ujenzi wa barabara. Kutsamiswa khuko kundalongoza kuhangamiza raslimali na chipato kama irivyoorodheshwa phapha tsini:

- Majengo na Nyumba
- Mihi
- Mabira
- Pato ra Chibiashara

**Jedwali ra Tsano (E): Muhtasari wa Athari kanda na Ardhi**

| # | Barabara | Idadi ya Biashara na sehemu za Makalo ga atu | Idadi ya atu andiohangamiza biashara na Makalo gao | Idadi ya atu andiohangamiza Mabira | Idadi ya Mbira | Idadi ya Mihi | Idadi ya Atu andiohangamiza Mihi |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Barabara ya Khwanza (A) | 1 | 1 | 0 | 0 | 10 | 2 |
| 2. | Barabara ya Nnne (D) | 1 | 0 | 1 | 1 | 10 | 3 |
| 3. | Barabara ya Tsano (E) | 25 | 18 | 2 | 5 | 2843 | 75 |
| | **Jumula** | **27** | **19** | **3** | **6** | **2,863** | **80** |

**Jedwali ra Sita (F): Vitengo vya Makundi vya Atu Ario na hali khomu Andioathirika na ujenzi wa Barabara**

| # | Vitengo vya Makundi ya Atu | Idadi ya Atu |
|---|---|---|
| 1. | Atu ario na Ulemavu wa Chimwiri | 1 |
| 2. | Atumia /Ario na Umri Ubomu | 5 |
| 3. | Ario Akongo Mahututi | 6 |
| 4. | Mayatima | 4 |
| 5. | Magungu | 2 |
| | Jumula | **18** |

**Mtazamo na Mpangiriro wa Chijumula wa Kutsamisha na Kupatira atu Makalo Mbadala wa Hahu (RAP 3)**

Mpangiriro wa Uhenzi Kazi wa 4.10 (OP 4.10) wa Bengi ya Dunia waorodhesha Jamii ya Duruma kukhala ndio atu chiasilia a sehemu yiyi na ndio andioathirika na ujenzi wa barabara khwa ajili ya Mradi uu. Na kwa sababu yiyo, jamii ya Chiduruma anastahili kupewa uangalifu wa chipekee tsini ya Mpangiriro uu dza viratu jamii ambayo inaishi kahi za hali khomu ya chimaisha. Mpangiriro na mikakati ya Jamii yiriyotengwa na yiishiyo katika mazingira makhomu (VMGP) wa Mtsara Ubomu wa Mwache watayarishwa ni Mradi wa Uhifadhi wa Madzi na Kudzikwamula Kulaana na Mabadiliko ga Hali ya Anga (Kenya Water Security and Climate Resilient Project – KWSCRP). Mpangiriro uo wachirirwa, uchihakikishwa na uchiidhinishwa ni Bengi ya Dunia na baadaye uchiikhwa wazi mwaka wa 2014. Vivyo be, utayarishaji wa Mpangiriro wa Mikakati wa Hahu watuwiriza khwa uphephi sana kanuni ambazo zaorodheshwa khwenye Mpangiriro wa uhendajii kazi wa Bengi ya Dunia OP 4.10 na OP 4.12. Chihususa Mpangiriro wa uhendaji kazi OP.4.10 unaeleza chikamili khwamba miradi yosi indiyofadhiliwa ni Bengi ya Dunia lazima yitie ndani mikakati ituwirizayo (a) khwepuka madhara mabomu khwa

jamii asili (b) Ichikala kayidimikika kuepuka madhara mabomu be kupatikane mbinu za kuphunguza, kukinja au kufidia athari ambazo zindasababishwa ni utekerezwaji wa mradi.. Kupatana na kanuni zizo, michoro ya barabara za Mwache zaangazira sehemu ambazo zakala za barabara ili kuziboresha na pharatu ambapho kaphakalire na barabara pho pindi be yo michoro ya barabara yalenga phatu ambapho kaphakalire na atu anji ili kuphunguza athari za utsamishaji. Ili kufikira uamuzi wa ni lwaphi ambapho phangefaa phakhale na barabara, khwahendeka mashauriano ga china phamwenga na jamii lengwa ili kupata phatu mwafaka khwa ujenzi wa zo barabara.

Mpangiriro wa uhendaji kazi OP.4.10 unaenderera kukazira khwamba "Ichikala kahi ya hali zisizo za kawaida kayiidimikika kwepuka kutsamisha atu, be yiye mwenye kuhitaji ardhi, kandafurusha atu bila kupata uungwaji mkono wa atu anji kulaa khwa atu hasa akaazi asilia ambao andaathirika khwa uo utsamishaji. Andioathirika na utsamishaji uo ni ashiriki khwenye sehemu ya mashauriano, gamapema, gawaziwazi, bila kushurutishwa ili kukale na makubaliano ga mapema. Baada ya mashauriano gago, kulingana na Mpangiriro huu wa Bengi ya Dunia OP 4.2, yiye mwenye kuhitaji ardhi yunapaswa kutayarisha mikakati na mipangiriro yindiyofungamana na mahitaji ga atu asili kutia ndani mikakati ya kupata ardhi mbadala baada ya uhamisho.

Pharatu yiidimikikavyo Mpangiriro wa kutsamisha na kutsakulira atu makalo ga mbadala, akaazi amuda ure anahenzekhana auye kwa ardhi na maeneo gao ga chiasili ichikala yo sababu ya kuihitaji ardhi yiyo indakala yisira.."

Katika hali yiyi ya Muradi wa Mwache, khwahendeka mazungumzo ga china na ure na walamu phamwenga na aratu ambao angeathirika na utsamishadzi khwa sababu ya utekelezwaji wa Muradi, na kupatana na mila na tamaduni za Aduruma. Timu ya utekelezwaji wa Muradi na enyeji abuni mikakati na mipangiriro ya utsamisadzi na kutsakhulira makalo mbadala kwa ajili ya aratu ambao angeathirika na utekelezwaji wa Muradi ambayo ingepatana na kanuni na tamaduni za Chiduruma. Hata vivyo baada ya gago mashauriano, aratu andioathirika apendelea apewe pesa zao khama maripho ili kufidia makalo ambago angehangamiza mbali na kugulirwa ardhi halafu atsamiswe. Khwa chifuti apendelea apewe pesa zao akadzipange mberembere ili adzitsakulire ardhi phophosi ahenzapho.  Pia yakubaliwa khukhala kukhale na chiwango cha pesa ambacho chindatengwa ili kufidia uvyalishadzi wa khwenye minda yao na kuaudzira hali yao ya kudzikimu chimaisha. Mpangiriro kabambe waikhwa khwa ajili ya aratu ambao angeathirika na utsamishadzi uo ili kuhakisha khwamba anadumisha hali yao ya chiutsumi, ikale akhala anategemea ardhi zao kudzipatira chipato au biashara zozosini zihusianazo na pharatu phatu ambapho andauswa. Mpangiriro uo wa kuaudzira enyeji hali yao ya kudzikimu chimaisha udzaambatanishwa khwenye Sura ya Nane dza Nakala ambatanishi Namba Mwenga I.

**Mashauriano kahi ya aratu atu andioaoathirika na utekelezwaji wa Muradi phamwenga na Ashikadau anjine.**

Ili Mpangiriro wa utsamishadzi na utsakulaji wa makalo mbadala ukhale na mafanikio na bila vikwazo vinji, kunahenzekana kukhale na mashauriano ga mara kwa mara na gakale na china na mare phamwenga na aratu andioathirika phamwenga na ashikadau anjine. Mashauriano gago ga china ganakusudiwa kujumulisha atu binafsi na makundi kahi za aratu andioathirika na utekelezwaji wa Muradi. Mashauriano gago ni muhimu sana khwa ajili ya kuhakikisha mafanikio ga mipango na utekelezaji wa Muradi na shuhuli zosini ambazo zina uhusiano na Muradi. Mikutano yiyo ya mashauriano phamwenga na ashikadau tafauti ambayo yatiya ndani kuikwa lwazu khwa Ramani na Michoro ya Barabara zosini, sehemu ambazo zingehitaji kurichwa wazi khwa ajili ya barabara yafanywa kuanzira tarehe chenda (9) Januari hadi Ishirini na Sita (26) Februari 2022.  Mashauriano phamwenga na aratu andioathirika na utekelezaji wa Muradi gahendwa khwenye mikutano ya Mabaraza na mahojiano ga mwenga khwa mwenga na ashikadau anjine na pia aratu ario na habari za ndani yahendwa kahi za maofisi gao. Hudhurio wakati wa

yiyo mikutano idzaambatanishwa khwenye Jedwali ambatanishi Namba Tsano na kumbukumbu zidzaambatanishwa khwenye Jedwali Namba Nne.

**Jedwali Namba Sabaa (G): Mikutano ya Mashauriano iriyofanywa kuhusiana na Muradi khwenye eneo ra Muradi.**

| # | Tarehe | Phatu pha Mikutano | Ache | Alume | Jumula |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | 15/2/2022 | Ofisi ya Chifu ya Vikinduni | 44 | 52 | 96 |
| 2. | 16/2/2022 | Ofisi ya Chifu ya Mnyezeni | 38 | 62 | 100 |
| 3. | 18/2/2022 | Ofisi ya Chifu ya Miyani | 24 | 36 | 60 |
| 4. | 23/2/2022 | Ofisi ya Chifu ya Chigato | 34 | 55 | 89 |
| 5. | 23/2/2022 | Ofisi ya Chifu ya Makutano | 19 | 29 | 48 |
| 6. | 23/2/2022 | Ofisi ya Chifu ya Mwashanga | 16 | 3 | 19 |
| 7. | 24/2/2022 | Kasemeni katika eneo ra Ofisi ya Frontman | 89 | 233 | 322 |
| 8. | 25/2/2022 | Soko ra Pemba Madukani | 28 | 46 | 74 |
| | | **Jumula** | **292** | **516** | **808** |

**Jedwali Namba Nane (H): Mikutano ya Mashauriano Phamwenga na Ashikadau Anjine**

| # | Tarehe | Madzina ga Ashikadau | Phatu Pha Mkutano | Idadi ya Atu Ariohudhuria |
|---|---|---|---|---|
| 1. | 09/1/2022 | Halmashauri ya Maenderero ga Pwani (CDA) | Khwenye Ukumbi wa Ofisi ya CDA | 12 |
| 2. | 10/1/2022 | Halmashauri ya Chitaifa ya Raslimali za Madzi (WRM) | Khwenye Ukumbi wa Ofisi ya WRM – Pwani | 4 |
| 3. | 10/1/2022 | Frontman | Kahi za Ukumbi wa Ofisi ya Frontman | 8 |
| 4. | 15/2/2022 | Mwakilishi wa Wodi Ya Kasemeni (MCA) | Khwenye Ukumbi wa Ofisi ya Frontman Kasemeni, Mwishimiwa. Anthony N. Yama | 5 |
| 5. | 24/2/2022 | Naibu wa Kamishena wa Kaunti (DCC) | Ofisi ya Naibu wa Kamishena wa Kaunti - Kinango | 4 |

| | | | | |
|---|---|---|---|---|
| 6. | 18/2/2022 | Mwavumbo | Madukani Makutano | 5 |
| 7. | 25/2/2022 | Msaidizi wa Kaunti Kamishena (ACC) | Ofisi ya Msaidizi wa Kaunti Kamishena Kasemeni | 3 |

**Jedwali ra Khwanza I: Muhtasari wa Hoja zirizozushwa baada ya Mikutano ya Mashauriano garigohendeka phamwenga na andioathirika na utekelezaji wa Muradi na Ashikadau tafauti tafauti.**

| # | Hoja | Maswali garigozushwa ni andioathirika (PAPs) | Majibu garigolaviwa /Mlonyuma |
|---|---|---|---|
| 1. | Ardhi ambazo enye kaapho kwa wakati uu | Indakaladze kwa ara amiliki a vipande vya ardhi ambao kaapatikhanire wakati wa kufanywa kwa mipangiriro ya utsamishadzi na kutsakula kwa makalo mbadala na pia wakati wa chipindi cha maripho ga fidia? | Tume ya Chitaifa ya Ardhi (NLC) indaika pesa zao za maripho kanda khwenye Akaunti ya chihicheye khwa ajili yao mpaka andiphopatikana, Akaunti yiyo yindakala inavyala faida. Yo Timu ya utekelezaji wa Mipangiriro ya Utsamishadzi na Utsakuladzi Makalo mbadala achisaidiana na Maofisa a Utawala kuchirira Ofisi ya Chifu andaenderera kuatsakula mpaka andiphopatikana. Andiphopatikana, andachizirwa khwenye mfumo wosini uriohumika ili aeleweshwe ndipho aphokere maripho gao. Aratu ambao kaandapatikana pesa zao zindaenderera kubaki kwa Akaunti yiyo. |
| 2. | Mabira garigo khwenye sehemu ya kandakanda ya barabara | Je kundakala na maripho ga mabira na mizimu yindiyopatikana kandakanda ya barabara? | Mila na desturi za Jamii zinaishimiwa sana na zindaishimiwa wakati wa utekelezaji wa Muradi, kwa vivyo mabira na mizimu yosini yindariphwa. Baada ya maripho ashiriki a jamii andahakikisha khwamba mabira na mizimu inatsamiswa kulingana na desturi za chijamii. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 3. | Kesi za urithi | Kesi nyinji za urithi wa ardhi bado kusikizwa na kwamulwa na khakuna vyeti vya kumiliki mashamba sambi indakaladze khwa maripho ga ara ambao arithishwa ardhi ni avyazi ambao afa na kakhukalire na makubaliano ga urithi? | Muradi undashuhulikira kesi za urithi zosi, yuyatu Wakili wa Muradi ambaye yunashuhulikira mambo ga urithi wa ardhi kahi za eneo ra Mradi, yiye ndiye ambaye yundakabidhiwa zizi kesi pia azishuhulikire. Wakili yundahakikisha khwamba aratu alengwa andaphokera barua zao za makubaliano ga maripho khwa ajili ya ardhi ya familia ili apate maripho kulaa khwa Tume ya Chitaifa ya Ardhi (NLC). Hata vivyo familia zaambirwa mapema kwamba atsagule mutu mmwenga yendiyeiwakilisha familia khwa upande wa maripho kwa niaba yao. Mwakilishi yiye yunahenzekana akale mwenye kuaminika chasi cha khwamba achiphokera maripho yundahakikisha khwamba chila mshiriki wa familia yundapata maripho ga khwakhwe kupatana na mukataba wao arioandikishirana. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | |
| 4. | Maripho ga Raslimali, mihi na mimera | Mimera, mihi na raslimali zinjine zindariphwadze? | Ardhi yosini, raslimali na mihi yindiyoathiriwa ni Muradi yindafidiwa chikamili. Hata vivyo mimera ya muda ufuti dza viratu matsere na maharaghwe kagandariphiwa, enye andapewa muda wa kuvuna mimera yao. Hangu yo mipangilio ya Muradi iriphoanzishwa na tarehe hususa kumanyiswa, andioathirka anaenderera kumanyiswa khwamba bado anaidima kwenderera kuphanda na kuvuna mimera yao ya muda ufuti kadiri anaenderera kugodzera maripho gao. Pia anaenderera kufahamishwa khwamba mimera yosini ya muda ure yindiyophandwa wakati wa chipindi chichi cha mpito kayindatarwa wala kufidiwa ni Tume ya Chitaifa ya Ardhi<br><br>Mpangiriro uu undahakikisha khwamba aratu andioathirika anaenderera kufaidika na ardhi yao khuno achingojera maripho iwapho gandachelewa na yindasaidia kuahakikishira khwamba khakuna uvamizi wa ardhi kulaa khwa atu anjine. Hata vivyo maripho gandiphofanywa, aratu andioathirika na utekelezwaji wa Muradi kaandaruhusiwa kuphanda chitu chochosi khwa sababu andatarajiwa kutsama, ila chisha andapewa muda ufaao ili avune na kuokola raslimali yoyosini ambayo yindakala yibaki khwenye ardhi yao ambayo andaitsama. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 5. | Mihi ya chiasili na iriyo na manufa ga chitiba | Je mihi ya Chiasili na iriyo na manufaa ga chitiba indarichwa khwa sababu inatimiza jukumu muhimu katika jamii? Khwa sababu inahumika dza dawa na manufaa ga chiibada.? | Kadiri yidimikikavyo Muradi undajaribu kuokola mihi dza yiyo, hata vivyo isiphoidimikika kwepukika be maripho galinganago na utamaduni gandalaviwa ili phatu phapho phahumike khwa ajili ya kutekeleza Muradi. Michoro yosi ya Barabara indaikhwa wazi kwa jamii ndo ichikhala kuna phatu ambapho ni mzukani pha chijamii au phana mihi ihumirwayo dza mizuka khwa makusudi ga ibada au inahumirwa khwa mambo ga chitiba be kukhale na mashauriano ga mapema kahi ya jamii na Timu iriyokabidhiwa madaraka ga utekelezaji wa Muradi ili phapatikane mwafaka ufaao ili maslahi ga Mradi na ga jamii gatirirwe maanani. |
| 6. | Vipande vya ardhi ambavyo vyathiriwa ni Mtsara Ubomu na Barabara khwa chivimwenga | Je kundakhala na maripho mara mbiri kwa ajili ya vipande vya ardhi ambavyo vindakhala khwenye barabara na khwenye Mtsara Ubomu? | Vipande vyosi vya ardhi ambavyo vindahitajika khwa sababu ya ujenzi wa Mutsara Ubomu wa Mwache vindafidiwa chikamili. Vipande viratu ambavyo kavindakala viriphiwa khwa sababu ya kesi zirizowasilishwa, pesa zao zindakhala khwenye Akaunti ya Chipekee mpaka malamishi gao gandiphosuluhishwa na fidia kulaviwa khwa amiliki. |
| | | | Maripho gandiphofanywa be arioathirika andapewa notisi na muda wa kutsama ili ardhi imilikiwe ni serekali. Khakundakala na maripho mara mbiri khwa ajili ya chipande chimwenga cha ardhi ila vipande vya ardhi ambavyo kavipho katika sehemu ya ziada ya barabara vindariphiwa bora vikhale kaviriphiwirwe mapema. |
| 7. | Maripho khwa ajili ya Miradi ambayo yatengezwa ni mashirika manjine ga Chiserekali khwenye eneo riro ra Muradi | Je Muradi undaripha jamii khwa ajili ya ardhi ambayo yaphalwa pindi khwa ajili ya ujenzi wa barabara na kaariphiwirwe pho pindi? | Swali riri rajibiwa ni Chifu wa sehemu yiyi ambaye waamanyisa enyeji khwamba Miradi yiyo yatekelezwa ni Serekali ya Kaunti ya Kwale. Miradi yiyo yatekelezwa khwa ajili ya kuafaidi anantsi ili kuvugula sehemu yiyi ili anantsi aidime kuchira khwa urahisi khwenye zizo barabara. Chifu waenderera kuafahamisha kukhala ni anantsi enye ambao akala alavya mapendekezo gago ga ujenzi uo wa barabara mapema khwa vivyo kayiidima kuriphiwa ni Tume Ya Chitaifa ya Ardhi (NLC) khwa sababu anantsi auya tena khwenye ardhi ambayo tayari akhala adziyilavya khwa serekali ambayo sambi yakhala ni mali ya serekali. Chifu wenderera kuaambira khwamba Miradi ya Barabara za Mtsara Ubomu Mwache ni tafauti na miradi ya barabara za Kaunti na iwapho ardhi, mihi, majengo na mimera indaathirika wakati wa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | ujenzi wa zizo barabara be zitariphiwa chikamili. |
| 8. | Maripho khwa ajili ya nyumba ambazo kazidzangwe kukamilika kujengwa | Je nyumba ambazo ambazo kazidzangwe kukamilika kujengwa pia nazo zitafidiwa ichikala zindaathiriwa ni ujenzi wa Barabara? | Nyumba zosini zindizoathiriwa ni ujenzi wa barabara za Mutsara Ubomu wa Mwache zindariphiwa chikamili, Chila nyumba indakala na maripho ga khwakhwe kulingana na yiyatu hatua ya ujenzi yondokala yifika. Chila nyumba yindahenderwa makadirio wakati ambapho awakilishi a Tume ya Chitaifa ya Ardhi andiphofika ili kuhenda ukaguzi. |
| 9. | Maripho ga sehemu ya Mtsara Ubomu ambago bado kufanywa | Kuna atu ambao kaadzangwe kuriphiwa khwa ajili ya ardhi ambayo yaphalwa kwa ajili ya ujenzi wa Mutsara Ubomu, indakhaladze khwao? Na sambi ichikhala kahi ya garatu makalo maphya ariphotsamira kumba ni phatu ambapho barabara indachirira Je andariphiwa mara ya phiri kwa ajili ya o Mtsara Ubomu na pia khwa ajili ya barabara? | Sehemu za ardhi ambazo zaphalwa kwa ajili ya ujenzi wa Mtsara Ubomu na barabara zindafidiwa chikamili. Wakati uu maripho ganaenderera kufanywa vivyo bee ni akale na subira. Wakati uu Serekali inashuhulikira maripho ga sehemu bomu muhimu za kwanza na phiri yaani P 1 na P 2. Aratu ambao aathirika na ujenzi uu na kaadzangwe kuriphiwa khwa ajili ya sehemu zosini mbiri na akhale na uhakika khwamba andariphiwa chikamili, na ichikala bado kuna malalamishi be oahusika naaende khwa Ofisi za atu a Frontman na za Serekali ili lalama zao zishuhulikirwe. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 10. | Maripho khwa ajili ya Raslimali ambazo bado zina mzozo | Indakhaladze kuhusu maripho khwa Raslimali ambazo zina mzozo kutia ndani sehemu ya mabira? | Vipande vyosini vya ardhi, Raslimali kutia ndani mabira ambago zina mzozo ni lazima mizozo isuluhishwe khwanza ndipho maripho gafanywe. Tume ya Chitaifa ya Ardhi (NLC) indaika pesa zizo khwenye Akaunti ya Chipekee. Timu ya utekelezaji wa Muradi phamwenga na Ofisi ya Utawala wa Serekali kuchirira Ofisi ya Chifu andakikisha khwamba mizozo yosini ya ardhi inasuluhushwa khwa wakati ili kuhakikisha khwamba utekelezaji wa Mradi kautatizwa. Aratu andioathirika na Muradi anashauriwa kutatua mizozo ya khwao ya ardhi kwa kuhumira mbinu za kusuluhisha mizozo zipatikanazo ko masinani kabila ya iyatu Timu ya kufanya ukaguzi kufika. Hata vivyo bado kuna nafasi ya kutatua mizozo yao kuchirira Kamati ya kutatua mizozo (Grievance Redress and Resettlement Committee - GRRC). |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 11. | Chiwango cha maripho ga Mbira na Mizuka | Kwa wakati uu maripho ga chila mbira ni shilingi 50,000 je chiwango cho kachiidima koonjezwa angalau chikafika 150,000? | Chicho chiwango cha shilingi 50,000 cha maripho khwa chila mbira chaikhwa ni Tume ya Chitaifa ya Ardhi (NLC ) na ni ao hichiyao ario na uwezo wa kubadilisha. Maripho ga mizuka ganatofautiana kulaa phatu phamwenga mpaka phanjine ichitegemea makubaliano na oenye mizimu yiyo ama jamii ya phatu phapho. Hata vivyo ni lazima kukale na uthibitisho na makubaliano kahi za ahusika na aimirizi a Mradi. |
| 12. | Madhara ga vumbi rilaaro khwenye eneo ra ujenzi wa barabara khwa ajili ya aratu ambao anaishi kandakanda ya barabara | Je jamii ambao anaishi kandakanda ya barabara andariphwa kwa sababu ya athari ya vumbi wakati wa ujenzi wa barabara? | Kakhuna maripho khwa ajili ya vumbi rindirotapakaa wakati wa ujenzi wa barabara, hata vivyo mikakati indaikwa ili kuphunguza madhara ga vumbi. Kahi ya yo mikakati iriyoikwa ni kunyunyiza madzi wakati wa ujenzi wa barabara ili kuphunguza vumbi na madhara ga khwakhwe. Ukaguzi wa athari za Chimazingira na Chijamii (Environmental and Social Impact Assessment – ESIA) wahendwa khare phamwenga na Mpangiriro wa Utsamishaji na kutsakula makalo mbadala na undaikwa wazi undiphoidhinishwa. Ukaguzi uu unalavya mwelekeo wa china wa hatua ambazo zinapaswa kuphalwa ili kuphunguza madhara ga vumbi na madhara manjine ga Chimazingira ambago gandalairira wakati wa ujenzi wa barabara. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 13. | Maripho khwa ajili ya ardhi iriyokodishwa | Chikala mutu wakodisha ardhi na achiphanda mihi, je yundariphwa? | Kahi za hali yiyi, yuyatu mwenye ardhi yundariphwa khwa ajili ya ardhi halafu yuyatu ariyekodisha yundariphwa khwa ajili ya mimera ariyoiphanda. Kwa vivyo kundakala na maripho mara mbiri tafauti, kwa ajili ya ardhi na mihi. |
| 14. | Mahitaji ga maripho | Ni matakhwa gaphigo ambago ganahitaji kutimizwa ili mutu ariphwe ni Tume ya Chitaifa ya Ardhi NLC? | Tume ya Chitaifa ya Ardhi NLC yindahitaji Stakabadhi zituwirizazo ili kuhenda maripho khwa ajili ya aratu arioathirika na ujenzi wa Mutsara Ubomu.:<br>Nakala ya Chitambulisho cha Chitaifa<br>Nakala ya Akaunti ya Bengi<br>Nakala ya cheti cha umiliki wa ardhi/Nakala ya Baruwa ya Umiliki wa Ardhi<br>Nakala ya cheti cha Halmashauri ya Kodi<br>Muradi undaasaidia aratu ambao aathirika kupata stakabadhi zizo khwa sababu kuna anjine ahangamiza vitambulisho vyao na tayari akala afahamishwa khukhala adzitahidi ili apate zizo Stakabadhi kabila ya maripho khwaanza. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 15. | Michoro na muundo wa barabara | Je barabara za Mradi wa Mtsara Ubomu wa Mwache zindatuwa mkondo wa zira barabara za Kaunti ama kuna barabara mbiphya ambazo zindaanzishwa? | Michoro na Muundo wa barabara indafunulwa wazi khwa aratu ambao andaathirkia na ujenzi kabila ya ukaguzi khwa ajili ya kutengeza mipangilio ya utsamishaji na utsakulaji wa makalo mbadala (RAP). Hata vivyo muundo wa barabara wa vivi undadumishwa na kuboreshwa kwa zizo barabara zinjine ilhali pia kundakala barabara mbiphya ambazo zindaundwa. Ichikala kundakala na mabadiliko katika muundo wa barabara be jamii yosi khwa ujumla indajulishwa na kueleweshwa kuhusu mabadiliko gago. |
| 16. | Maripho khwa ajili ya ardhi ambazo kazina vyeti vya umiliki wa ardhi | Je ara atu andioathiriwa ni Muradi na khaana vyeti vya umiliki wa Ardhi andariphwa pia? | Wizara ya Madzi kuchirira Wizara ya Ardhi indahakikisha kukhala atu osi andoathiriwa ni Mradi ana vyeti vya Umiliki wa Ardhi ili aidime kufidiwa ni Tume ya Chitaifa ya Ardhi NLC. Aratu ambao kaandakhala na vyeti khwa sababu ardhi yao yikahi za hatua ya upimadzi, be Mradi undapata Stakabadhi zizo za upimadzi kulaa khwa Ofisi za Kaunti za upimadzi wa Ardhi ili kusaidia kutengeneza maripho khwa ajili ya aratu andioathirika. Kwa aratu ambao andakala ahangamiza vyeti vyao vya umiliki wa Ardhi khwa sababu mwenga au yinjine, Mradi undasaidia kupatikana kwa Kadi za Chijani Chitsi kama ziihiwavyo ni atu a Ardhi zihenderwe ukaguzi katika Ofisi za Ardhi halafuye zindawasilishwa kwa Tume ya Chitaifa ya Ardhi (NLC) kwa ajili ya maripho. |
| 17. | Maripho khwa ajili ya Ardhi ambayo ni ya avyaazi ijapokuwa khuna ana ambao pia andaathirika | Je ara ana ambao andakala ajenga khwa ardhi ambayo ni ya avyazi ao andafidiwa pia? | Wakati wa ukaguzi wa Raslimali zirizoko khwenye ardhi yindiyohitajika, aratu osi ambao andakala na majengo khwenye yiyo ardhi be zindaandikishwa chihicheye dza atu andioathirika na Mradi pia. Khwamba nao pia anafuzu kupata maripho khwa ajili ya raslimali zizo ijapokuwa ajenga khwenye ardhi ambayo ni ya avyazi ao. Sheria yatambua riro jambo chimberembere chimapema na ichiika mikakati ya maripho tafauti kwa chila yeyosini yuyatu ambaye yundakhala yujenga khwa ardhi zizo bora ithibitishwa khwamba raslimali yiyo ni yakwe, khwamba nao pia ana haki ya kudai maripho ili afidiwe. . |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 18. | Kuhangamiza mapato khwa sababu ya utsimbaji wa mawe au mtsanga khwenye sehemu ambayo yindaphalwa khwa ajili ya ujenzi wa Mtsara Ubomu na barabara. | Je vijana ambao akala achidzishuhulisha na utsimbaji wa mawe au mtsanga kama njira yao ya kudzipatira chipato katika Maisha gao andariphwa kwa sababu ya kukosa tegemezo rao ra chimaisha wakati sehemu yiyo indaphalwa khwa ajili ya utekelezaji wa Mradi? | Kuhangamiza khwa chipato khwa sababu ya ujenzi wa Mtsara Ubomu na shuhuli zinjine ambazo zinauhusiano na ujenzi uo zashulikirwa na zinjine zinaenderera kushuhulikirwa ili kuhakikisha khukhala kakuna yeyosini andiyehangamiza uwezo wa khwakhwe wa kudzikimu chimaisha. Baada ya kuhakikishwa khwa shughuli zizo za chimapato ambazo zikhala zichifanyika katika eneo ra Mradi ni Tume ya Chitaifa ya Ardhi NLC, osini andioathirika andafidiwa chikamili ili atsakhule shuhuli zinjine za kudzipatira mapato. Biashara zosi na njira za kudzipatira mapato chimaisha zindaandikishwa na kuhakikishwa kabila ya maripho kufanywa. |
| 19. | Walamu na ure wa barabara zihusianazo na Mtsara Ubomu wa Mwache na tarehe ya khwanza kwa Mradi. | Barabara za Mtsara Ubomu wa Mwache zindakala na ure na walamu chasi chani? Ni wakati wani Mradi undaanza na ni wakati wani ara arioathirika andapata maripho ga khwao? | Miundo na Michoro ya barabara zizo indaikhwa wazi kwa jamii. Ujumbe katika stakabadhi zizo zinaonyesa ure, walamu na phatu ambapho barabara zizo zindaundwa. Kuhusiana na mwanzo wa Mradi, Jamii yaelezerwa uo wakati wa mwanzomwanzo kabisa wakati wa kutengeza Mipangiriro na Mikakati ya kutsamisa na kutsakula makalo mbadala (RAP). Mipangiriro yiyo ya RAP indiphoidhinishwa be indajulishwa khwa jamii na NLC indaidhinisha chirasmi maripho khwa ajili ya aratu andiooathirka na ujenzi wa Mradi. |
| 20. | Khwandikwa kazi khwa vijana kulaa khwenye eneo ra utekelezaji wa Mradi na ujenzi wa barabara | Je vijana a eneo rino ra khwehu andaajiriwa kazi wakati wa ujenzi wa barabara za Mtsara Ubomu wa Mwache? | Kazi zosi zirizopho katika Mradi zindatangazwa waziwazi katika majukhwaa tafauti tafauti. Kama irivyo desturi ya Miradi minji ya Serekali khwanza andatsakhula aratu osini ario na ujuzi wa kutengeza zizo shuhuli kulaa katika jamii zirizo khwenye eneo riro ra Muradi khwanza andapewa kipaombele kabila ya kutsakhula katika maeneo ga konze. Ichidzakhala kaandapata ndipho andatsakulwa konze ya yiyo jamii. |
| 21. | Kufidiwa khwa sehemu za makumbusho ga utamaduni wa Chijamii | Je Mradi undafidia gharama zindizohusika katika kutsamisa sehemu za kumbukumbu za utamaduni wa Chijamii na sehemu za mahumizi ga umma ambazo zindaathirika wakati wa kujengwa kwa | Ardhi zosi kutia ndani mabira, mizimu na sehemu za mahumizi khwa ajili ya Umma ambazo zindaathirika khwa sababu ya utekelezaji wa Mradi zosi zajumulishwa khwenye maripho. Khwa vivi gharama zosini za kutsamisa mabira na mizimu zajumulishwa khwenye maripho. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | barabara za Mradi wa Mwache? | |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 22. | Kufaidika kulaana na ujenzi wa Mtsara Ubomu | Mradi uno undajengadze uwezo wa vijana ili aidime kuvuna matunda ga kutekelezwa khwa Mradi baada tu Mradi kukamilika? | Wizara ya Madzi, Usafi wa Mazingira na Unyunyirizadzi Madzi Mashambani kuchirira khwa Halmashauri ya Chitaifa ya Ujenzi yaandaa mafundisho khwa ajili ya vijana katika Nyanja tafauti tafauti dza viratu ujenzi wa majengo yaani ujenzi kwa kuhumira mawe, ufundi wa Sitima, Ufundi wa Mifereji na kadhalika. Lengo bomu ra kuandaa mafundisho gaga ni ili kuajenga vijana uwezo mapema khwa taaluma na ujuzi mbalimbali ambao ungehitajika wakati wa utekelezaji wa Mradi. Kwa vivyo be yakhala ujuzi uo uasaidie kupata kazi wakati ujenzi unaenderera. Vijana pia anaidima kuhumira ujuzi uo ili kudzifaidi maishani na kudziphenyeza katika shuhuli ambazo zindaapatira mapato maishani mwao, hali yiyo andaidima kudzikimu phamwenga na famila zao hata baada ya kukamilika khwa Mradi. Vijana ndio anji na ndio andohitajika khwa unji wakati wa utekelezaji wa Mradi. Wakati wa utekelezaji wa Mradi andadzipatira ujuzi aina mbalimbali ambao undaasaidia khwenye sehemu tafauti tafauti za kazi hata baada ya Mradi kukamilika khwa sababu ya utajiri wa ujuzi ambao andakhala apata khwa andakhala apanua uwezo wa khwao wa kupata ajira. Wakati Mtsara Ubomu undiphokamilika kundakala na fursa zinjine za kuajiriwa au kudziajiri, khwa mfano andaidima kudzitia khwenye ukurima wa mimera yenye mapato ga dzulu, uvuvi ama katika Nyanja ya utalii na kudzistarehesha. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 23. | Dhuluma za Chijinsia , ariotengwa na atu andioathirika na utekelezaji wa Mradi ambao anaishi na hali khomu za Chiutsumi | Kuna njira ziphizo za kuhakikisha usawa ambazo zaikwa ili kurinda ario khwenye ndoa hasa anaache atsilafiwe manufaa ga maripho ga raslimali zirizophalwa ni Mradi ili nao afaidike na kuarinda kulaana na ufujaji na kutengwa atsipate manufaa ga fidia na vivyo kuaricha hohehahe? | Mradi una jukumu na Mamlaka ga kuhakikisha khwamba familia ambazo zindaathirika na utekelezaji wa Muradi kazirichwa taabuni khwa sababu ya shuhuli za Muradi. Dza irivyofanywa khwenye Sehemu bomu muhimu ya khwanza naya Phiri (P1 na P2) kahi za Mpangiriro wa Mikakati ya Utsamishadzi na Utsakulaji wa Makalo Mbadala wa Kwanza RAP 1 ambapho ahusika andaphokera maripho gao na kutsamira makalo maphya, familia zashauriwa kuvugula Akaunti za Bengi za phamwenga ili kuhakikisha khwamba shuhuli zosi zihusuzo maripho na mahumizi ga pesa za fidia zinafanywa baada ya makubaliano ga phamwenga. Mshauri wa Mradi wahusika phabomu sana kuhakikisha khwamba jambo riro rihendeka, hali yiyi yasaidia phabomu kuphunguza migogoro ya mahumizi mabaya ga pesa za maripho kwa sababu aratu osini ambao anahusika anamanya chila hatua yendererayo na khakuna pesa ambayo yindalaviwa kabila ao kuhusishwa na kukubaliana kuhusu mahumizi ga pesa. Mbinu yiyo yiyo ndio yindiyohumirwa katika maripho khwa ajili ya sehemu za Barabara za Mwache. Zaidi ya vivyo chila mmwenga kahi za aratu andioathirika na utekelezaji wa Mradi andahitajika kutayarisha Mpangiriro wa Chibinafsi ya viratu ambavyo andahendera pesa ili kudzimudu maishani mwao kabila ya kuphokera maripho kulaa khwa Tume ya Chitaifa ya Ardhi NLC. Mpangiriro uu usaidia phabomu kuphunguza hatari ya ufujaji wa pesa za fidia. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 24. | Fidia khwa ajili ya ahenziabiashara ambao anafanyira kazi kahi za maduka ambago ni ga kukodisha | Je ara ambao anahenda biashara kahi za maduka ambago ni ga kukodisha andariphwa pia khwa sababu ya kuathirika na utekelezaji wa Mradi? | Aratu ahendao biashara kahi za maduka ga kukodisha phamwenga na biashara zinjine ambao andaataathirka khwa sababu ya ujenzi wa barabara za Mwache pia nao andafidiwa khwa sababu Maisha ni lazima gaenderere au audzirwe kahi za hali yao ariokala kabila ya utekelezaji wa Mradi. Andariphiwa kwa miezi mihahu ya chiratu chipato chao ambacho anapata khwa mwezi khwa sababu ya kuhangamiza chipato chao kulaana na biashara zao.. |

| | | | |
|---|---|---|---|
| 25. | Maripho khwa ajili ya aratu ambao agula ardhi lakini kaadzangwe kubadilisha vyeti vya umiliki vya ardhi ili visome madzina gao na ambao pia andaathirika na utekelezaji wa Mradi | Ni anoani andioriphwa ichikala kuna atu ambao agula ardhi na bado vyeti kavidzangwe kubadilishwa ili visome madzina gao au shuhuli ya utsamishaji bado kukamilika? | Katika hali yiyi aratu arioguza ardhi kaandaphokera maripho khwa ajili ya ardhi ambayo akala adziiguza kare. Aratu amiliki aphya ambao agula ndo andiopewa maripho gago. Na ichikala mwenye kuguza ardhi kadzangwe kubadilisha umiliki wa ardhi khwa yiye muguli muphya be yundahitajika atiye saini ya makubaliano khwamba ye muguli wa ardhi yuna haki ya kuphokera maripho gago. Makubaliano gaga gandaimirirwa ni Wakili wa Mradi na gandatiywa saini ni ye muguzaji na ye muguli wa ardhi halafu stakabadhi zizo zosini phamwenga na zinjine ambazo zinahitajika zindakabidhiwa Tume ya Chitaifa ya Ardhi ili kushuhulikira maripho khwa ajili ya yuyatu mmiliki mphya wa ardhi. Hata vivyo iwapho mwenye yiyatu ardhi yundakahala kutia saini makubaliano gago be chipande chicho cha ardhi chindaorodheshwa khukhala china mzozo. Tume ya Chitaifa ya Ardhi NLC ina mfumo unjine wa kushuhulikira kesi zizo kabila ya maripho kufanywa. Pia kuna ura mfumo wa kutatua mizozo (GRM) urionakiliwa khwenye Sura ya Chenda ya Mpangiriro wa Mikakati ya Utsamishadzi na Utsakulaji wa Makalo Mbadala (RAP) undahumika ili kutatua uu mzozo na ni lazima kukhale na uthibitisho wa ugulaji kulaa khwa yuyatu mwenye kudai kwamba wariphira yo ardhi yiyo wakati wa kutatua mzozo uo kuchirira mfumo wa kutatua mizozo wa GRM. |
| 26. | Maamuzi ga chiwango cha Maripho ga Fidia. | Chiwango cha Maripho ga Fidia chindaamulwa namuna yanii? | Muradi waandika kazi ataalamu ario na ujuzi hususa wa kuhenda ukaguzi wa thamani ambao anafanya kazi tsini ya Mshauri wa Muradi (RAP Consultant) ambao aidhinishwa chirasmi chisheria ni Halmashauri ya Chitaifa ya Ukaguzi wa Thamani. Ataalamu aa ana uwezo wa kuhenda ukaguzi wa thamani wa ardhi, majengo, mihi, mimera, raslimali za chiukoo/Chijamii khwa ajili ya Mpangiriro wa Utsamishaji na Utsakulaji wa Makalo Mbadala RAP. Wakati wa ziara ya khwanza Utathmini undakala ni khwa sababu ya kutengeza bajeti ya mfumo wosini wa utekelezaji wa Mradi.<br><br>Kujumulishwa khwa chiwango chosi hususa cha pesa zindizohitajika ili kufidia atu kundahendwa ni Tume ya Chitaifa ya Ardhi NLC khwa sababu ao ndio ario na jukumu riro chisheria kupatana na Sheria ya Ardhi. Chiwango halisi cha maripho khwa chila chipengele na raslimali zindizoathirika wakati wa utekelezaji wa Muradi chindaikwa ni Tume ya Chitaifa ya Ardhi NLC wakati wa |

| | | | |
|---|---|---|---|
| | | | khwanza khwanza kabisa wa utekelezaji wa Mpangiriro wa Utsamishaji. Chiwango halisi cha maripho chindaerekezwa ni thamani ya bei zirizoko sokoni khwa wakati uu halafu kundafanywa ukarabati chidogo ili kujumulisha chiwango cha pesa ili kugharamia kuyugwa khwa aratu andiotsama khwenye makalo gao ili kutsakula makao mbadala ambacho chinakadiriwa kukhala ni aslimia kumi na tsano (15%) ya chiratu chiwango cha raslimali chindichofidiwa. Chiwango chicho chindariphwa chijumla dzulu ya garatu maripho manjine ga kufidia raslimali na vivyo gakale maripho kamili ga fidia. Mpangiriro uu unaambatana kabisa na mwerekezo uriolaviwa khwenye jedwali ra Chiratu ambacho ni Haki ya Mutu kufidiwa (Entitlement Matrix). Khuna gharama zinjine za ziada ambazo Mradi undagharimia ambazo zinatia ndani usafirishaji wa waathiriwa khwenda khwenye makalo gao maphya na gharama za ubadilishaji wa vyeti vya umiliki wa ardhi kulaa khwa enyeji hadi kwa Mradi, zizi zosi zindajumuishwa phamwenga ili kufikira gharama kamili za utekelezaji wa Muradi. |

**Tarehe Hususa za Utekelezaji wa Mipangiriro**

Tarehe hususa za Mpangiriro wa Mikakati Namba Tahu (RAP 3) wa Mwache kufungwa ni tarehe 26 Februari, 2022. Tarehe yiyi yaikhwa wazi khwa uma kahi ya sehemu zosi ambazo Mradi ungefika na khwa atu osi ambao angeathirka na utekelezaji wa Mradi uu. Aratu ariohusika kahi za uhamasishaji uu akala ni Mshauri wa Mradi phamwenga na awakilishi a utawala ya Wizara ya Ndani na Usalama wa Chitaifa. Nia ya uhamasishaji uu wakala kuamanyisa anantsi matukio muhimu na kabila ya kufanywa khwa usoroveya wa china wa nyanjani. Ujumbe uu wachizwa wakati wa mabaraza ga umma na pia khwa atu binafsi ariopatikana kho midzini khwao wakati wa ukaguzi uo wa china. Anantsi aelezwa waziwazi khwamba aratu andiotsamira kuphenya kahi za eneo ra mradi na aratu ambao andahenda maenderero manjine khwa yiyo ardhi baada ya tarehe yiyo kaandapata maripho gogosini na kwamba ajidzilazimisha kutsamira kuphenya khwenye eneo be indakala kainabudi auswe bila maripho gogosini kutia ndani majengo gao.

Kulingana na kanuni za uhendaji kazi wa Bengi ya Dunia OP 4.12, tarehe yiyo ya mwisho ndo wakati hususa ambapho ukaguzi wa china unafanywa ili kuhenda utathmini wa china. Tarehe yiyo ni muhimu khwa sababu inarinda na kuzuia atu kutsamira khwenye eneo ra Mradi ambaro ringeonjeza gharama za kufidia ambazo zinapaswa kuepukwa. Atu ambao andatsamira kuphenya khwenye eneo ra Mradi baada ya tarehe yiyo be kaandapata maripho gogosini khwa ajili ya ardhi na raslimali zao zindizokala khwenye ardhi yiyo. Tarehe yiyo pia ni muhimu khwa sababu miphaka ya eneo ra Mradi indaikhwa wazi kabila ya ukaguzi wa china wa atu na raslimali ijapokuwa phapho nyuma tayari zakhala zidziikwa wazi khwa umma, indasaidia kwepusha utsamiraji wa atu anji katika eneo na kudai maripho ga uwekezaji wa tamaa.

**Ukaguzi wa Thamani na Maripho ga Fidia**

Raslimali ambazo zindaathiriwa ni ujenzi wa barabara za Mwache ambazo zinaidima kufidiwa ni kama zituazo:

i. Ardhi
ii. Majengo
iii. Mihi
iv. Mbira
v. Mapato kulaana na biashara

Raslimali zosi zizo zakaguliwa na zichipewa thamani ya khwakhwe nayo ichikala msingi wa kuhenda maripho kamili, yiyi shuhuli yafanywa ili kuhenda makadirio ga gharama ya kufidia wakati wa kuhenda mipangiriro ya mapema.

**Kanuni na Mikakati ya kuhenda maripho**

Mpangiriro wa Utekelezaji wa Mikakati ya uhamisho RAP unanuia kuhakikisha kukhala aratu osini ambao aathirika na utekelezaji wa Mradi anafidiwa chikamili na asaidiwe kuuyira hali ya khwao ya kawaida ya chimaisha dza viratu arivyokhala kabila ya utekelezaji wa Mradi ama hata akale bora Zaidi kuriko vyo arivyokala pindi.

**Kustahili kupata maripho**

Maripho gastahiligo ganategemea namna na mfikiro wa hasara ambayo mtu yundapata khwa kuuswa pharatu phatu ambapho udziphabara ambapho mutu yunaishi. Atu osini andioathiriwa ni utekelezaji wa Muradi anastahili kupata maripho na kusaidiwa kupata makao mbadala kuambatana na Mfumo wa Uhendaji Kazi wa Bengi ya Dunia OP 4.12 na Sheria za Kenya. Hata vivyo inamanyikana kukala kuna anjine ambao andaathirika ambao

kaana stakabadhi ambazo zinatambulika chisheria ili kustahili maripho khwenye ardhi ambayo anaishi kahi za eneo ra Mradi. Khwa vivyo be maripho katika Mpangiriro uu wa Utekelezaji RAP undategemea phabomu Mpangiriro wa uhendaji kazi wa Bengi ya Dunia OP. 4.12 ambao unaelezera khwa undani Zaidi hali za anantsi kuriko sheria za Kenya kuhusiana na aratu ambao anadai haki ya maripho kahi za mazingira gaga.

Khwa vivyo aratu atu andiouswa kahi za makazi gao aikwa kahi za makundi mahahu dza idzivyoelezwa phapha tsini:

i. Aratu atu ambao ana uthibitisho wa haki ya kumiliki ardhi kuchirira stakabadhi (kutia ndani chiukoo na chijamii dza irivyotambuliwa ni sheria za Kenya)
ii. Aratu atu ambao kaana stakabadhi wala uthibitisho wa chisheria kwa ardhi ambayo anaishi vivi kare wakati ukaguzi undiphoanza lakini ana haki ya kudai maripho khwa ajili ya ardhi na raslimali ambazo anamiliki kwa vivi bora tu ikale haki zizo zinatambuliwa ni sheria ya Kenya au haki zizo zindatambuliwa na kuthibishwa wakati wa utekelezaji wa Mpangiriro wa RAP.

iii. Avamizi asio halali ambao avamia sehemu ya ziada ya barabara ambapho anahendera biashara tsini ya majengo ga muda mfuti. Wakati wa ukaguzi yathibitishwa kukhala kuna boma mwenga ambaro rina atu ane a familia ambao andaathirika na utekelezaji wa Mradi wa barabara za Mradi kwenye Barabara A ambao anahenda biashara kahi za eneo ra akiba ra barabara..

**Mfumo wa Umiliki wa Ardhi kahi za eneo ra Mradi**

Mfumo wa Umiliki wa Ardhi kahi za eneo riri ra Mradi ni huru kwa mahumizi ga mutu chibinafsi kama ahenzavyo. Vivyo be kupatana na mfumo uu atu osini andioathirika anastahili kuphokera maripho. Aratu arioandikishwa dza enye ardhi chitamaduni ni vitswa vya familia ambao anji ni analume na ndo ambao apendekezwa kuphokera maripho. Hata vivyo timu ya utekelezaji wa Mpangiriro uu wa RAP andahenda kazi kwa phephi na ashiriki osini a familia na Tume ya Chitaifa ya Ardhi NLC ili kukale na makubaliano na uwiano wa ugavyaji wa pesa kahi ya ano baba, ache ao na ana ao ambao anastahili. Zaidi ya riro ario kahi za ardhi ya familia zizo lakini afanya miradi/kujenga chibinafsi kahi za ardhi andapata maripho gao chivyao. Miradi yiyo inatia ndani majengo na mihi.

Mpangiriro uu wa RAP unatambua khwamba uhalisi uu uhendwa vikomu ni Sheria ya Ardhi ambayo inatambua ario na vyeti vya umiliki wa ardhi khwamba ndio anastahili kufidiwa. Hata vivyo Mpangiriro uu wa RAP unatambua khwamba hata aratu ambao andaathirika hata kala khaana vyeti vya umiliki wa ardhi ambavyo vina madzina gao pia nao ana haki ya kupata fidia chiukamili khwa ajili ya ardhi, majengo na mihi na riri raorodheshwa tototo sana khwenye Ratiba ya Maripho.

**Mtazamo na Mpangiriro wa Maripho ga Fidia**

*(i) Maripho ga Ardhi*

Maripho ga chipesa gandafanywa mwenga kwa mwenga ni Tume ya Chitaifa ya Ardhi khwa aratu ambao andakala aidhiinishwa kukhala ni amilki a ardhi iriyophalwa ni muradi, ama khwa aratu awakilishi ambao andakala adziidhinishwa ni Korti kuchirira haki za umiliki kahi za kesi ambazo zindahusu umiliki wa Ardhi ambao enye ni afadzi. Mradi undaajiri Wakili

andiyesaidia kuhakikisha khwamba ubadilishaji wa umiliki wa ardhi unahendwa khwa utaratibu wa chisheria kutia ndani kutsagulwa kwa awakilishi a ardhi za chibinafsi andioathirika na utekelezaji wa Muradi.

*(ii) Maripho ga Majengo, Mimera, Mihi na Mbira*

Maripho khwa ajili ya majengo, mimera, mihi na mbira gandahendwa chiukamili khwa pesa taslimu zindizoriphiwa mwenga khwa mwenga kwa ariothsagulwa kuphokera maripho gago. Maripho gago gandahendwa ni Tume ya Chitaifa ya Ardhi NLC.

*(iii) Maripho khwa ajili ya Mradi wa Kuudzira atu Hali yao ya Kudzikimu Chimaisha*

Mifumo tafauti tafauti za kuudzira atu hali yao ya chiutsumi zindahumika (Livelihood Restoration Programmes - LRP) na Wizara MoWSI achishirikiana na Idara mbalimbali za chiserekali, na uongozi wa chijamii wa mashinani. Utekelezaji wa Mufumo uu undaambatanishwa na kukalapho kwa raslimali, maarifa, ujuzi na uzoefu wa chila familia. Hatua zindizophalwa katika utekelezaji wa Mfumo wa Hahu RAP 3 khwa ajili ya aratu andioathirika na Mradi zinafungamana na shuhuli ambazo anahenda khwa wakati uu ambazo zina uhusiano wa mwenga khwa mwenga na mambo ga chirimo. Vivyo basi andaphokera usaidizi wa mambo ga chirimo na biashara. Pia andaphokera mafunzo ga msingi ga khwiimirira pesa ili aidime kuhumira pesa andizophokera khwa busara na zizidi kuvyalana kwa unji kuchirira kuekeza tototo.

Mpangiriro uu una vipengele vihahu:

(i) Kujengwa uwezo wa chirimo/ Kupata usaidizi wa kudzikimu chimaisha kulaa khwa ardhi;

(ii) Mafundisho ga kuimirira mahumizi ga pesa;

(iii) Kusaidiwa kwaanzisha biashara

**Mfumo wa Kuwasilisha na Kutatua Mizozo (Grievance Redress and Management – GRM)**

Mfumo uu wa kuwasilisha na kutatua mizozo ni muhimu sana ili kuruhusu aratu andioathirika na utekelezaji wa muradi kuwasilisha malalamishi gao kuhusu mchakato wosini mzima wa kutsamisha na kutsakhulira atu makao mbadala. Malalamishi gachiwasilishwa mapema be inakala rahisi sana khwa hatua za chiharaka kuphalwa na marekebisho gafaago kutekelezwa khwa uharaka. Mfumo uu ni muhimu ili kusaidia khukhale na uwazi kahi za umiliki wa ardhi na utsakulaji wa makao mbadala. Timu iriyopewa jukumu riri andahakikisha khwamba malalamishi gosi gandashuhulikirwa kabila ya khwaanza kwa Mradi na manjine pia gandasuluhishwa kadri ganalairira.

Mfumo urio lwazu wa kushuhulikira malalamishi ni muhimu sana khwa sababu unalavya fursa na jukhwaa ra kuwasilisha malalamishi na kupatikana khwa suluhu ra haraka na khwa wakati ufaao. Mfumo uu ni muhimu khwa sababu atekelezaji a Muradi anapata mwanya wa kutambua vyanzo vya malalamishi khwa wakati ufaao na kuruhusu suluhisho ripatikane khwa uwazi na uwajibikaji. Malalamishi gosi dzulu ya maripho ga ardhi gana uwezekano ubomu wa kulairira wakati na baada ya kutekelezwa kwa mikakati ya Mradi.

Ukosefu wa uwazi unalongoza khwenye hatua za kutsaaminiana na kunaongoza khwenye kuhenda maamuzi gatsigofaa khwa pande zosi mbiri. Mfumo wenye kuimirirwa tototo na uriothibitishwa wa kutatua mizozo unatsangira mahusaiano madzo kahi ya atekelezaji a Mradi na jamii ihusikayo na vivyo be kweepuka uhasama kati ya pande zosi na zinaongoza kwa Mradi kufanywa khwa wakati uriopangwa kabila na baada ya mwanakandarasi kukabidhiwa khwa eneo ra Muradi.

Mradi uu wa Mtsara Ubomu wa Mwache tayari una mufumo uu thabiti wa kuphokera na kutatua mizozo. Mfumo uo wafanikiwa kutekeleza majukumu ga khwakhwe ambao kufikira vivi ufanikiwa kutatua malamishi na mizozo kulaana na utekelezwaji ambao unaenderera wa Mipangiriro na Mikakati wa Kwanza RAP 1a na 1b. Mfumo uo wa kuphokera na kutatua malalamishi mwanzo wa mwaka huu wapanuliwa ili kutia ndani kushughulikira ujenzi wa Mtsara Ubomu  na undapanuliwa Zaidi ili ushughulikire lalama zozosini zindizodzilavyira wakati wa utekelezaji wa Mpango wa Phiri na wa Hahu. Hata vivyo Mfumo uu wa malamishi undaonjezwa ashiriki zaidi kulaana na aratu ambao andaathitika na ujenzi wa barabara za Mwache.

**Jedwali ra Kumi (J): Uhendaji kazi wa Mfumo wa Kuphokera na Kutatua Mizozo**

| # | Phatu pha kuphirika malalamishi | Idadi Malalamishi garigo phokerwa | Lalama zirizosulu-hishwa | Chiwango cha suluhisho (Asilimia) | Lalama ambazo kazidzangwe kukamilishwa |
|---|---|---|---|---|---|
| 1. | Chidzidzini | 154 | 154 | 100% | 0 |
| 2. | Kata Tide | 17 | 17 | 100% | 0 |
| 3. | Taarafa (Kaunti Tide) | 109 | 90 | 83% | 19 |
| | Jumula | **280** | **261** | **93%** | **19** |

Kama idzivohadzwa mapema mfumo uu wa kutatua mizozo undapanuliwa ili kuonjezera anachama anjine kulaa khwa aratu andioathirika na ujenzi wa barabara. Lengo bomu ra kufanya vivyo ni ili kuhakikisha khwamba kuna Mpangiriro urio lwazu na wenye kuthibitishika na kutuwirizika ambao lalama zilairirazo khwa sababu ya utekelezaji wa Mradi zinatuwiriza uo mkondo wa kuphokera lalama kulaa khwa mutu binafsi/boma, isikizwe na uamuzi ulaviwe. Kusikizwa na kuamulwa kwa malalamishi kunaidima kufanywa khwa chikao ambacho si rasmi ama kuchirira njira mbadala za kutatua mizozo bora zifungamane na utaratibu ufaao chisheria wa kusuluhisha mizozo na dza irivyoelezwa khwenye mfumo wa uhendaji kazi wa Bengi ya Dunia OP 4.12 na ukale unatimiza vigezo virivyoikhwa vya ubora na utaratibu urivyoikhwa. Hata vivyo ichikala enye mizozo kaaridhikire be anaidima kutuwiriza mfumo wa chisheria wa kuphirika kesi mahakamani khwa sababu ii ndiyo njira idziyobaki na ni haki ya chila mmwenga ambaye yunaona khwamba maamuzi gadzigofanywa mashinani kagamridhishire.

Mfumo wa sambi wa kutatua mizozo wa Mradi wa Mwache una vitengo au ngazi vitsano vya kusuluhisha migogoro dza idzivyoorodheshwa phapha:

1) Kamati ya Atumia ya Kusuluhisha mizozo ya ardhi za Chidzidzini
2) Kamati ya Kata Tide ya Utsamishaji na kutsakula Makao mbadala phamwenga na kuphokera na kusuluhisha mizozo.

3) Kamati ya Taarafa/Kaunti Tide ya Utsamishadzi na kutsakula Makalo mbadala phamwenga na kuphokera na kusuluhisha mizozo
4) Kamati ya Kutatua Mizozo khwenye Kaunti
5) Kuchirira Koti au Mahakama khwenye Koti ya Mazingira na Ardhi ambazo zabuniwa mwaka wa 2012 tsini ya sheria ya Mazingira na Ardhi ya 2012. Mahakama zizo zabuniwa ili kushughulikira mizozo ihusianayo na mambo ga ardhi. Vivyo be aratu andioathirika na utekelezwaji wa Muradi achoona kukhala kaadzangwe kuridhishwa ni maamuzi ga viratu vitengo vinjine be ahuru kutuwiriza utaratibu wa chisheria kotini wakati wowosini uratu.

**Mfumo wa Kuudzira arioathirika uwezo wao wa Kudzikimu chimaisha**

Mpangiriro wa chibinafsi wa chila nyumba ili kuaudzira uwezo wao wa kudzikimu chimaisha ni lazima uambatanishwe na stakabadhi zinjine na kuphirikhwa kwa Tume ya Chitaifa ya Ardhi NLC kabila ya maripho kufanywa. Hali yiyi inalenga kuhakikisha ya khwamba pesa za maripho zinarindwa ili ziidime kuhehera na kushughulikira hali ya chila familia isiuye khwenye hali ya uchochole baada ya kuphokera pesa zao za maripho na uwezo wao wa kudzikimu chimaisha. Mahumizi madzo ga pesa zirizotengwa khwa ajili ya kuyuudzira famila uwezo wakhwakhwe wa kudzikimu chimaisha ndiro lengo ra msingi ra Muradi uu baada ya kutsamiswa kulaa khwa eneo ambaro akala adziribara kulaa hangu pindi. Lengo riri rinafungamana kabisa na uratu Mpangiriro wa Mikakati RAP 1 na 2 khwenye jedwali ra kustahili maripho, na ichikala madhara ga utsamishaji uo si ubomu kwa Maisha ga familia chiutsumi be Tume ya Chitaifa ya Ardhi NLC indalavya tu pesa bila mipangilio ya ziada ya kudzikwamula na riri rindahendeka ichikala inahusisha biashara za vivi vivi tu.

Iyatu Timu ya Utekelezaji wa Mipangilio ya Utsamishaji RAP indaongoza katika kuhakikisha khwamba chila familia anatengeza mpango wao chibinafsi wa kudzikwamula chiutsumi baada ya kutsama. Zaidi ya riro aratu andioathirika na Mpangiriro wa Mfumo wa Hahu RAP 3 andajumulishwa kahi za kutambua miradi ya chijamii ambayo inaidima kutekelezwa katika jamii ambayo andakala atsamira. Aathiriwa ao pia andafaidika na mafundisho ga kujengwa uwezo na apatirwe pembejeo zindizoasaidia kuanzisha tena luphya shuhuli zindizoasaidia kudzikwamula chiutsumi. Andaphokera huduma za chibiashara na chitaaluma ambazo zipangwa kutekelezwa tsini ya mwavuri wa Kudzikwamula chimaisha wa Mradi wa Mtsara Ubomu wa Mwache. Mifano ya huduma na shuhuli za kudzikwamula chiutsumi ambazo zinaidima kutekelezwa, malengo gao na kanuni zihusikazo za kwerekeza zidzoorodheshwa na kwelezwa tototo kahi za Sura ya Nane ya Ripoti ya Mipango ya Utekelezaji wa Muradi..

**Mpangiriro wa Taasisi ambazo zinahusishwa kahi za utekelezaji wa Mradi**

Mpangiriro uu wa Hahu wa Mikakati RAP 3 undatekelezwa ni Taasisi ambazo zajukumiwa kare kwa utekelezaji wa Mradi wosi wa Mtsara Ubomu wa Mwache kwa ujumula. Kundakalaa na Taasisi mbalimbali ambazo zindashirikiana chila mwenga yina majukumu ga Khwakhwe ili kufanikisha utekelezaji wosini wa Mradi wa Mtsara Ubomu wa Mwache. Taasisi zizo zinatia ndani za Chiserekali kulaa khwa Kaunti, Kaunti Tide na kulaa khwa Serekali kuu, Taasisi za Chiufundi, Ashauri kutia ndani a Chibinafsi na makampuni ga kulavya ushauri wa chiufundi na ushauri ambao osini aajiriwa ni Wizara ya Madzi.

Taasisi ambazo kufikira vivi zahusishwa ili kufanikisha utekelezaji ni dza zituazo:

a) Kulaa khwa Serekali Kuu – Wizara ya Madzi, Usafi wa Mazingira na Unyunyirizadzi Madzi Mashambani
b) Mradi wa Chitaifa wa Uhifadhi wa Madzi na Kudzikwamula kulaana na athari za Mabadiliko ga hali ya Anga (Kenya Water Security and Climate Resilience Project-KWSCRP) -Kulaa chitengo cha Serekali Kuu na Kulaa Eneo ra Pwani.
c) Chitengo cha Chitaifa cha Kuhakikisha Usalama wakati wa Utekelezaji wa Miradi

d) Mshauri wa Kubadilisha Umiliki wa Ardhi
e) Mshauri wa Utekelezaji wa Mradi RAP
f) Kamati ya Kuphokera Malalamishi na Kutatua mizozo
g) Kamati Bomu ya utekelezaji wa Mradi

**Ratiba ya Utekerezaji wa Mradi RAP**

Muda ambao waratibiwa kukamilishwa utekelezaji wa Mradi wakadiriwa khukhala miezi 24, hata vivyo shughuli za kuaudzira arioathirika uwezo wa khwao wa kudzikimu chimaisha ni khwenda ukaphala muda ure Zaidi na ufuatilizi pia unenda khwa muda Zaidi ya uratu wa kutsamisha na kutsakulira makalo mbadala (Tafadhali chirira Jedwali ambatanishi namba sita ili kudzifahamisha na ratiba yiyo).

Kutuwiriza ili kuhakikisha utekelezaji wa garatu ambago gapangwa ndo jambo muhimu sana kahi za Mpangiriro uu wa Mikakati yaani RAP. Kundakala na utuwirizaji mara mbiri- wa ndani na wa konze.

(i) Utuwirizaji wa ndani na kulavya ripoti

- Kutuwiriza shughuli za ujenzi
- Kutuwiriza shuhuli na kutimizwa khwa vigezo virivyoikwa khwa ajili ya Utsamishaji na Makalo mbadala

(ii) Utuwirizaji wa Konze na Kulavya Ripoti

- Ukaguzi kulaa khwa Mkaguzi Mshauri ariyejukumiwa kuhakikisha utekelezaji wa shuhuli zosi za Mradi
- Kuikwa wazi kwa Ripoti za ukaguzi
- Mkaguzi huru wa Jopo ra Chitaalamu ra Chimazingira na Chijamii

**Kuikwa Lwazu khwa Mpangiriro wa Mikakati wa Utsamishadzi na Kutsakula Makalo Mbadala RAP**

Mpangiriro wa Chimikakati RAP undaikhwa lwazu kwa lugha ya Chizungu na Muhtasari wa Mambo Mabomu (ambayo si ya Chitaalamu) indatafsiriwa katika lugha ya Chiswahili na Chiduruma. Tafsiri za Chiswahili na Chiduruma katika nakala ya maandishi indalaviwa dza vitabu khwenye chila nyumba kwa aratu ambao andakala adzaathirika na garigomo gandaaelezwa chinaganaga wakati wa mikutano phamwenga na agwiradau anjine yindiyofanywa khwanzakhwanza ya kutsamisha atu kuhusu utekelezaji wa Mpangiriro wa Mikakati Namba Tahu RAP 3. Nakala ya Chizungu yindaikhwa lwazu kahi za mtandao chielektroniki za Taasisi zituwirazo: -

a) Mradi wa Chitaifa wa Uhifadhi wa Madzi na Kudzikwamula kulaana na athari za Mabadiliko ga hali ya Anga (KWSCRP)
b) Halmashauri ya Maenderero ya Eneo ra Pwani
c) Wizara ya Madzi, Usafi wa Mazingira na Unyunyirizadzi Madzi Mashambani
d) Serekali ya Kaunti ya Kwale
e) Chitengo cha Maswala ga Konze ya Bengi ya Dunia

Nakala za Vitabu pia zindapatikana katika ofisi zidzizoorodheshwa phapho dzulu kama ituwavyo:

a) KWSCRP Ofisi za Nairobi
b) KWSCRP Ofisi za Pwani
c) Ofisi ya CDA
d) Makao Mabomu ga Kaunti ya Kwale

e) Ofisi ya Mwanakandarasi
f) Ofisi za Kaunti Tide ya Kwale
g) Ofisi zosi za Lokesheni/Kata ambako kuna atu arioathirika na ujenzi wa Mradi
h) Ofisi zosi za Wodi ambako kuna atu arioathirika na ujenzi wa Muradi

**Bajeti ya Utekelezaji wa Mpangiriro wa Mikakati wa Hahu RAP 3**

Jumula ya pesa yindiyohitajika kwa utekelezaji wa Mpangiriro uu wa Mikakati Namba Tahu ni Milioni Mia Mbiri Kumi na Chenda, Magana Manane Themanini na Tsano Elfu, na Magana Mahahu Sitini na Tsano za Kenya. (**219,885,365)** kutia ndani pesa za kuyugwa khwa atu andiphokala anatsamishwa kulaa khwenye makalo gao ga asili kutsamira sehemu zinjine, pesa za kuudzira jamii uwezo wao wa kudzikimu Chimaisha, pesa za kushuhulikira ubadilishaji wa umiliki wa ardhi na za kutatua mizozo. Zaidi ya riro chiwango cha Asilimia 15 chatengwa ili kushughulikira shuhuli za phapha na pharatu za chiofisi, kutia ndani ufuatilizi wa utekelezaji wa Mradi na Utathmini au Ukaguzi baada ya kukamilika kwa Mradi. Gharama zosini zihusianazo na utekelezwaji wa Mpango uu wa Mikakati zidzoorodheshwa kahi za jedwali K phapha tsini zindashughulikirwa ni Chitengo cha kuimirira utekelezaji cha Mradi wa Chitaifa wa Uhifadhi wa Madzi na Kudzikwamula kulaana na athari za Mabadiliko ga hali ya Anga. Hata vivyo gharama ni khwenda zikabadilika khwa sababu ya hali ya bei ya bidhaa sokoni, vivyo basi Tume ya Chitaifa ya Ardhi NLC ina jukumu ra kufanya marekebisho ga Bajeti wakati wa mwanzomwanzo wa utekelezaji wa Mradi ili iambatane na hali halisi irivyo sokoni.

**Jedwali namba 11 - K: Muhtasari wa Makadirio ga Maripho ga Fidia khwa ajili ya andioathirika na Mradi kwa Mpangiriro Namba Tahu RAP 3**

| Barabara | Thamani ya Ardhi (Ksh) | Thamani ya Majengo, Uchigo (Ksh) | Thamani ya Biashara (Ksh) | Thamani ya Mihi na Uchigo wa Mihi Hai (Ksh) | Thamani ya Raslimali zindizoathirika (KSh) | Gharama za Kuyugwa @ 15% (KShs) | Makadirio ga Gharama zosi (Ksh) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|
| A | **233,027** | 20,000.00 | 20,000 | 13,000 | 286,027 | 42,904 | 328,931 |
| D | 1,295,943 | 70,000.00 | 0 | 0 | 1,365,943 | 204,891 | 1,570,835 |
| E | 91,453,742 | 14,401,200 | 180,000 | 6,404,100 | 112,439,042 | 16,865,856 | 129,304,898 |
| **JUMULA** | **92,982,713** | **14,491,200** | **200,000** | **6,417,100** | | **17,113,652** | **131,204,665** |

**Jedwali la 12 - L: Jumla ya Bajeti ya Utekelezaji wa Mpango wa RAP 3**

| # | Maelezo ga gharama kulingana na Chitengo | Gharama (KSh) |
|---|---|---|
| 1. | Ardhi | 92,982,713 |
| 2. | Majengo | 14,491,200 |
| 3. | Kuhangamiza Pato ra Chiutsumi | 200,000 |
| 4. | Mihi | 6,417,100 |
| **5.** | **Jumula Tide ya Khwanza 1** | **114,091,013** |
| 6. | Gharama ya Uyugaji (15%) | 17,113,652 |
| **7.** | **Jumula Tide ya Phiri 2** | **131,204,665** |
| 8. | Miradi ya kuudzira atu hali yao ya chiutsumi | 15,000,000 |
| 9. | Maripho ga Wakili kwa ajili ya kushughulikira vyeti vya Umiliki wa Ardhi | 30,000,000 |
| 10. | Ukaguzi huru baada ya utekelezaji wa Mradi | 10,000,000 |

| | | |
|---|---|---|
| 11. | Kushughulikira Mizozo | 5,000,000 |
| **12.** | **Jumula Tide ya Hahu** | **60,000,000** |
| **13.** | **Jumula Tide ya 2 + 3** | **191,204,665** |
| 14. | Matukio gasigotazamiwa (15% ya gharama ya utekelezaji wa RAP) | 28,680,700 |
| **15.** | **Jumula kamili ya Bajeti ya Utekelezaji wa RAP 3** | **219,885,365** |

**Hatua/Vihendo ambavyo serekali indabidi ifanye ili kuwezesha utekelezaji**

i. Maripho ga fidia kwa wakati ambao unafaa: Serekali yatenga pesa khwa ajili ya kuafidia aratu ambao andaathirika na utekelezaji wa Mradi, vivyo be maripho gago ganapaswa gahendwe khwa wakati ambao waratibiwa.

ii. Upatikanaji wa ahenzi akazi: Ili kufanikisha utekelezaji wa Mradi uu inahitajika ahenzi akazi akutosha apatikane khwa wakati ufaao na Wizara ifanye mipangilio istahiliyo kumpata Mshauri wa Utekelezaji wa Mpango uu namba Tahu kwa wakati baada tu ya Mpangiriro uu kuidhinishwa ni Bengi ya Dunia. Pia Serekali inapaswa kudzizatiti kumreha Mjuzi wa Mambo ga kuhakikisha usalama wa Chijamii andiyelavya mwerekezo na kuimirira utekelezaji wa Mpangiriro uu wa mikakati RAP.

**ZAMCONSULT CONSULTING ENGINEERS LTD**